JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MTIHANI WA KUMALIZA ELIMU YA MSINGI (PSLE) 2020

# MAARIFA YA JAMII

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MTIHANI WA KUMALIZA ELIMU YA MSINGI 2020

# MAARIFA YA JAMII

*Kimechapwa na:*
Baraza la Mitihani la Tanzania,
S. L. P. 2624,
Dar es Salaam, Tanzania.

© **Baraza la Mitihani la Tanzania, 2020**

Haki zote zimehifadhiwa.

YALIYOMO


DIBAJI ........ iv

1.0 UTANGULIZI ........ 1

2.1 Sehemu A ........ 2

2.1.1. Kipengele I: Uraia ........ 2

2.1.2. Kipengele II: Historia ........ 17

2.1.3. Kipengele III: Jiografia ........ 34

2.2 Sehemu B ........ 50

2.0 UCHAMBUZI WA UFAULU WA WATAHINIWA KATIKA KILA MADA ........ 58

3.0 HITIMISHO ........ 61

4.0 MAPENDEKEZO ........ 62

KIAMBATISHO ........ 64

## DIBAJI

Baraza la Mitihani la Tanzania limeandaa Taarifa ya Uchambuzi wa Majibu ya Maswali ya Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi mwaka 2020 kwa somo la Maarifa ya Jamii . Taarifa hii ina lengo la kutoa mrejesho hususan kwa watahiniwa, walimu, watunga sera, watunga mitaala na wadau wengine wa elimu. Matokeo ya uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika mtihani yamewezesha kupata taarifa kuhusu ujuzi na maarifa waliyokuwa nayo watahiniwa katika kipindi cha miaka saba ya Elimu ya Msingi.

Katika taarifa hii, uchambuzi wa kila swali umefanyika ambapo changamoto mbalimbali walizozionesha watahiniwa wakati wa kujibu maswali zimeainishwa. Aidha, ulinganifu wa kiwango cha ufaulu kati ya mwaka 2019 na 2020 kwa kila mada umefanyika ili kuonesha kupanda au kushuka kwa kiwango cha ufaulu katika kila mada. Chati inayoonesha ulinganifu wa ufaulu imewekwa mwishoni mwa taarifa hii.

Vilevile Uchambuzi unaonesha kuwa watahiniwa waliopata alama za juu walikuwa na maarifa yaliyowawezesha kubaini matakwa ya maswali wakati watahiniwa wenye uelewa mdogo hawakuweza kubaini matakwa ya maswali. Kimsingi, watahiniwa wengi waliopata alama za chini waliandika majibu yasiyo sahihi na wengine hawakujibu baadhi ya maswali au walichagua jibu zaidi ya moja, kinyume na maelekezo ya mtihani.

Baraza la Mitihani Tanzania lina imani kuwa mrejesho huu utawawezesha wadau mbalimbali wa elimu kuchukua hatua madhubuti ili kuboresha ufundishaji na ujifunzaji. Ni matumaini ya Baraza la Mitihani kuwa mamlaka husika zitahakikisha kuwa changamoto zilizoainishwa katika taarifa hii zinapatiwa ufumbuzi ili kuongeza maarifa na ujuzi kwa watahiniwa wa Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi.

Mwisho, Baraza la Mitihani linapenda kutoa shukrani za dhati kwa Maafisa Mitihani, na wengine wote waliohusika katika kuandaa taarifa hii.

**Dkt. Charles E. Msonde**
**KATIBU MTENDAJI**

## 1.0 UTANGULIZI

Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi (PSLE) ulifanyika tarehe 7 na tarehe 8 ya mwezi Oktoba , 2020. Katika mtihani huo, somo la Maarifa ya Jamii lilifanyika tarehe 8/10/2020. Jumla ya watahiniwa 1,023,950 walisajiliwa kufanya mtihani huu ambapo watahiniwa 1,008,268 sawa na asilimia 98.5 walifanya mtihani huo katika somo la Maarifa ya Jamii. Uchambuzi wa majibu ya mtihani wa Maarifa ya Jamii unaonesha kuwa watahiniwa 824,077 sawa na asilimia 81.73 % walifaulu mtihani huo katika somo hilo.

Somo la Maarifa ya Jamii katika mtihani wa PSLE lilikuwa na jumla ya maswali 40 ya kuchagua na 5 ya majibu mafupi yaliyokuwa yamegawanyika katika sehemu kuu mbili: A na B. Sehemu A ilikuwa na maswali 40 ya kuchagua ambayo yalikuwa yamegawanyika katika vipengele vitatu. Kipengele cha I: Uraia kilichokuwa na maswali 12, kipengele cha II: Historia kilichokuwa na maswali 14 na kipengele cha III: Jiografia kilichokuwa na maswali 14. Sehemu B ilikuwa na maswali 5 ya majibu mafupi ambayo ni swali 1 la Uraia, maswali 2 ya Historia na maswali 2 ya mwisho ya somo la Jiografia.

Watahiniwa walitakiwa kujibu maswali yote kutoka katika sehemu zote mbili. Aidha, katika swali la 1 - 40 watahiniwa walipewa machaguo matano katika kila swali, ambayo kati yake kulikuwa na jibu sahihi. Watahiniwa walitakiwa kuchagua jibu sahihi na kisha kuweka kivuli katika herufi ya jibu sahihi katika fomu maalum ya kujibia (OMR). Katika kujibu swali la 41 – 45, watahiniwa walielekezwa kuandika majibu yao katika nafasi zilizoachwa wazi kwa kutumia kalamu ya wino wa bluu au mweusi.

Katika taarifa hii, herufi ya jibu sahihi imewekewa alama ya nyota (*) katika majedwali na chati. Zaidi ya hayo, asilimia ya watahiniwa ambao hawakufuata maelekezo ya namna ya kujibu swali iliwekwa katika uchambuzi na kupewa jina “Mengine” ikimaanisha watahiniwa ambao hawakujibu kabisa swali husika au walichagua jibu zaidi ya moja kama inavyoonekana katika majedwali na chati. Katika uchambuzi huu, idadi ya watahiniwa na asilimia yao katika kila chaguo umeoneshwa. Ubora wa kiwango cha ufaulu kwa watahiniwa katika kila swali utategemea idadi ya watahiniwa waliochagua jibu

sahihi. Katika uchambuzi huu pia, sababu za watahiniwa kuchagua jibu, kuandika jibu sahihi au vipotoshi zimebainishwa.

Katika uchambuzi huu, ukokotoaji wa kiwango cha ufaulu unategemea idadi ya watahiniwa waliochagua au kuandika jibu sahihi kama ifuatavyo; endapo watahiniwa asilimia 0 hadi 39 ndio watakaokuwa wamechagua au kuandika jibu sahihi, ufaulu katika swali au mada hiyo utaelezwa kuwa ni hafifu. Kwa upande mwingine, endapo watahiniwa kati ya asilimia 40 hadi 59 watakuwa wamechagua au kuandika jibu sahihi, ufaulu katika swali hilo utaelezwa kuwa ni wa wastani. Aidha, ufaulu katika swali au mada utaelezwa kuwa mzuri endapo watahiniwa asilimia 60 au zaidi watakuwa wamechagua au kuandika jibu sahihi.

## UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA KILA SWALI

### 2.1 Sehemu A


#### 2.1.1. Kipengele I: Uraia

**Swali la 1:** Ni nani anahusika kumchagua Mwenyekiti wa kijiji?

A Wananchi wote katika kijiji
B Wajumbe wa kamati za kijiji
C Halmashauri ya kijiji
D Baraza la madiwani
E Wakuu wa idara za serikali katika kijiji

Swali hili lilitoka katika mada ya *Uongozi wa Serikali za Mitaa katika ngazi ya Mtaa/ Kijiji* na lililenga kupima uelewa wa watahiniwa kuhusu namna Mwenyekiti wa kijiji anavyochaguliwa. Kiwango cha ufaulu cha watahiniwa katika swali hili kilikuwa kizuri ambapo watahiniwa 859,267 (84.82%) waliweza kuchagua jibu sahihi A, *Wananchi wote katika kijiji.* Watahiniwa hawa waliweza kubaini kundi lenye sifa ya kumchagua mwenyekiti wa kijiji kwa sababu walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu taratibu za uchaguzi katika ngazi ya kijiji. Chaguzi zingine za viongozi zinazoendeshwa nchini Tanzania ni pamoja na uchaguzi wa Madiwani, Wabunge na Rais kwa kuzingatia Katiba ya nchi na miongozo mbalimbali inayotolewa

na Tume ya Taifa ya Uchaguzi. Chati Na.1 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali la 1.




**Chati Na. 1:** *Ufaulu mzuri wa watahiniwa katika swali la 1*

Aidha, watahiniwa 50,957 (5.03%) walichagua kipotoshi B, *Wajumbe wa kamati za kijiji*. Watahiniwa waliochagua kipotoshi hiki hawakufahamu kuwa wajumbe wa kamati za kijiji hawana mamlaka ya kuchagua Mwenyekiti wa kijiji. Watahiniwa hao walitakiwa kujua kuwa kazi ya wajumbe wa kamati za kijiji ni kuishauri Halmashauri ya kijiji kuhusu jambo lolote linalohusu majukumu ya Kamati za kijiji ambazo ni pamoja na kamati ya fedha, kamati ya huduma za jamii na kamati ya ulinzi na usalama.

Watahiniwa 43,616 (4.31%) waliovutiwa na kipotoshi D, *Baraza la Madiwani* hawakuwa na ufahamu wa muundo wa uongozi wa serikali ya kijiji. Baraza la madiwani si sehemu ya uongozi wa serikali ya kijiji bali ni ngazi ya juu ya uongozi wa serikali za mitaa inayoundwa na madiwani kutoka katika kata mbalimbali za Halmashauri katika Wilaya, Jiji au Manispaa, na jukumu lake kubwa ni kutunga sheria ndogondogo katika halmashauri ya wilaya, jiji au manispaa husika.


Watahiniwa 35,133 (3.47%) walivutiwa na kipotoshi C, *Halmashauri ya kijiji* kwa kuwa Halmashauri ya kijiji ni chombo kikuu cha utendaji katika kijiji hivyo kudhani kuwa Halmashauri ya kijiji ingeweza pia kuwa na mamlaka ya kumchagua mwenyekiti wa kijiji. Mwisho, chaguo E, *Wakuu wa idara za serikali katika kijiji* liliwavutia

watahiniwa 20,097 (1.98%) ambao hawakuwa na ufahamu wa taratibu za kidemokrasia za uchaguzi wa mwenyekiti wa kijiji. Wakuu wa idara za serikali katika kijiji ni waajiriwa wa mkurugenzi mtendaji wa halmashauri au serikali kuu. Hivyo, hawahusiki katika kumchagua mwenyekiti wa kijiji.

**Swali la 2:** Lipi kati ya yafuatayo ni jukumu la Baraza la Madiwani katika Manispaa?

A Kukusanya kodi katika Manispaa husika
B Kutunga sheria ndogondogo katika eneo lao
C Kuajiri mkurugenzi mtendaji wa Manispaa
D Kusimamia shughuli za uchaguzi wa mitaa
E Kuajiri wakuu wa idara katika Manispaa

Swali hili lilitoka katika mada ya *Serikali za Mitaa* na lilipima maarifa ya watahiniwa kuhusu majukumu ya Baraza la madiwani katika Manispaa. Ufaulu katika swali hili ulikuwa mzuri kwani watahiniwa 630,718 (62.26%) waliweza kubaini jibu sahihi B, *kutunga sheria ndogondogo katika eneo lao.* Watahiniwa walikuwa na ufahamu wa mamlaka waliyopewa madiwani ya kutunga sheria ndogondogo katika maeneo yao zinazowawezesha kutekeleza sheria mama zilizotungwa na bunge. Lengo la sheria hizi ndogondogo ni kuharakisha maendeleo katika eneo husika. Chati Na. 2 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali la 2.




**Chati Na. 2:** *Ufaulu mzuri wa watahiniwa katika swali la 2*

Aidha, watahiniwa 138,896 (13.71%) walivutiwa na chaguo A, *kukusanya kodi katika Manispaa.* Watahiniwa waliochagua kipotoshi hiki hawakuwa na ufahamu wa majukumu ya Baraza la Madiwani. Baraza la Madiwani si chombo cha utendaji wa shughuli za kila siku za Manispaa bali ni chombo cha uwakilishi cha wananchi na kiungo kati ya wananchi na Manispaa. Watahiniwa 133,241 (13.15%) walichagua kipotoshi D, *kusimamia shughuli za uchaguzi wa mitaa.* Hawakujua kwamba usimamizi wa chaguzi mbalimbali hufanywa na mkurugenzi wa halmashauri au manispaa kwa niaba ya Tume ya Uchaguzi ya Taifa. Watahiniwa 59,881 (5.91%) walivutiwa na kipotoshi C, *Kuajiri Mkurugenzi Mtendaji wa Manispaa,* huenda kwa sababu ya ukweli kwamba Mkurugenzi Mtendaji ni Katibu wa vikao vya Baraza la Madiwani hivyo kudhani kwamba anaweza kuajiriwa na Baraza la Madiwani. Hatimae, kipotoshi E, *kuajiri wakuu wa idara katika Manispaa,* kilivutia watahiniwa wachache zaidi 44,431(4.39 %) ambao hawajui taratibu za ajira katika mfumo wa serikali za

**Swali la 3:** Ipi kati ya zifuatazo ni faida za mfumo wa vyama vingi vya siasa nchini Tanzania?

A Kuongezeka kwa ajira serikalini
B Kutokuwepo kwa tofauti za kisiasa nchini
C Vyama vyote vya siasa kupokea ruzuku
D Kuongezeka kwa uwajibikaji serikalini
E Kuongezeka kwa wawekezaji toka nje

**Jedwali Na. 1: Idadi na asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo**

| Machaguo | A | B | C | D* | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 181,310 | 177,886 | 117,531 | 444,799 | 82,936 | 8602 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 17.90 | 17.56 | 11.60 | 43.91 | 8.19 | 0.85 |

Swali lilitoka katika mada ya *Demokrasia* na lilipima uelewa wa watahiniwa kuhusu faida za mfumo wa vyama vingi vya siasa nchini Tanzania. Kama Jedwali Na. 1 linavyoonesha, ufaulu katika swali hili ulikuwa wa wastani ambapo watahiniwa 444,799 (43.91%) waliweza kubaini jibu sahihi D, *kuongezeka kwa uwajibikaji serikalini.* Watahiniwa hao walikuwa na uelewa juu ya faida za ushindani wa vyama vingi vya siasa nchini Tanzania. Vyama vya upinzani

hufuatilia utendaji na uwajibikaji wa chama cha siasa kilichopo madarakani na serikali yake, hali ambayo husaidia kuongezeka kwa uwajibikaji wa watendaji wa serikali. Faida nyingine ni kulindwa kwa haki za binadamu, kuwepo kwa uwazi, kupungua kwa vitendo vya rushwa na kuimarika kwa utawala wa sheria.

Aidha, watahiniwa 181,310 (17.90%) walivutiwa na chaguo A, *kuongezeka kwa ajira serikalini.* Watahiniwa hao hawakuelewa kuwa ongezeko la ajira ni matokeo ya kukua kwa shughuli za kiuchumi katika nchi na hakuna uhusiano wa moja kwa moja na uwepo wa mfumo wa vyama vingi. Watahiniwa wengine walivutiwa na kipotoshi B, *kutokuwepo kwa tofauti za kisiasa nchini.* Watahiniwa hawa hawakufahamu kuwa ushindani wa vyama vingi vya siasa hauondoi tofauti za kiitikadi miongoni mwa vyama vya siasa kwani kila chama cha siasa kinaamini katika mrengo wake wa kisiasa.


Watahiniwa 117,531 (11.60%) waliovutiwa na kipotoshi C*, Vyama vyote vya siasa kupokea ruzuku* walikosa ufahamu kuhusu utaratibu wa vyama vya siasa kupata ruzuku. Sheria ya vyama vya siasa inataja vyama pekee vyenye uwakilishi katika bunge na udiwani ndivyo vinavyostahili kupata ruzuku. Mwisho, watahiniwa wachache 82,936 (8.19%) waliovutiwa na kipotoshi E, *kuongezeka kwa wawekezaji toka nje* hawakufahamu kuwa, pamoja na mambo mengine sambamba na hali ya utulivu wa kisiasa, wawekezaji wanavutiwa na uwepo wa sheria mbalimbali zinazolinda mitaji yao, miundombinu rafiki ya kufanya biashara, uwekezaji, na uwepo wa utawala wa sheria.

**Swali la 4:** Ni mwaka gani Umoja wa Mataifa (UN) ulipitisha Azimio kuhusu Haki za Binadamu?

A 1964 B 1945 C 1948 D 1961 E 1984

Swali lilitoka katika mada ya *Misingi ya Demokrasia* na lilipima uelewa wa watahiniwa kuhusu mwaka ambao Azimio la Umoja wa Mataifa (UN) la Haki za Binadamu lilipitishwa. Ufaulu wa watahiniwa ulikuwa hafifu kwani watahiniwa 255,047 (25.18%) tu waliweza kubaini jibu sahihi C, *1948.* Watahiniwa waliochagua jibu sahihi walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu tarehe za mikataba mbalimbali muhimu ya kimataifa inayosiamamia na kutetea haki za

Binadamu. Chati Na 3 inaonesha ufaulu dhaifu wa watahiniwa katika swali la 4.




**Chati Na. 3**: *Ufaulu dhaifu wa watahiniwa katika swali la 4*

Aidha, watahiniwa wengi 307, 447 (30.35%) walivutiwa na kipotoshi B,*1945* huenda kwa sababu mwaka 1945 Umoja wa Mataifa ulianzishwa. Kutokana na muktadha huo, walidhani Azimio kuhusu Haki za Binadamu lilipitishwa mwaka huo pia. Watahiniwa 175,961 (17.37%) walivutiwa na kipotoshi A, *1964.* Watahiniwa 120,817 (11.93%) walichagua kipotoshi D, *1961,* na *watahiniwa* 142,696 (14.09 %) walichagua kipotoshi E, *1984.* Watahiniwa waliochagua A, D na E walivutiwa na machaguo hayo huenda kutokana na miaka hiyo kuwa pia ni ya matukio muhimu katika historia ya nchi yetu. Kwa mfano kipotoshi A, *1964,* ni mwaka ambao Tanganyika na Zanzibar ziliungana na kuwa nchi moja Tanzania. Tukio hili huenda limehusishwa na watahiniwa waliokosa maarifa ya kutosha na azimio la umoja wa mataifa kuhusu haki za binadamu. Kipotoshi D*, 1961* ni mwaka ambao Tanganyika ilipata uhuru wake, na kipotoshi E*, 1984* ni mwaka ambao katiba ya Tanzania kwa mara ya kwanza iliweka kipengele cha kulinda haki za binadamu.

**Swali la 5:** Kwa nini tarehe 7 Aprili ya kila mwaka inakumbukwa nchini Tanzania?

A Ni siku ya kifo cha Rais wa kwanza wa Zanzibar Abeid Karume.

B Ni siku ya kifo cha Rais wa kwanza wa Tanzania Julius K. Nyerere.

C Ni siku ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar.

D Ni siku ya kuzaliwa TANU.

E Ni siku ya uhuru wa Zanzibar.

**Jedwali Na. 2: Idadi na asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo**

| **Machaguo** | **A*** | **B** | **C** | **D** | **E** | **Mengine** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 446,505 | 197,870 | 172,638 | 132,070 | 53,272 | 10,709 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 44.07 | 19.53 | 17.04 | 13.04 | 5.26 | 1.06 |

Swali lilitoka katika mada ya *Alama za Taifa* na lilipima uelewa wa watahiniwa kuhusu kumbukumbu ya tarehe 7 Aprili inayoadhimishwa kila mwaka nchini Tanzania. Kama Jedwali Na. 2 linavyoonesha ufaulu katika swali hili ulikuwa wa wastani ambapo watahiniwa 446,505 (44.07%) waliweza kubaini jibu sahihi A, *Ni siku ya kifo cha Rais wa kwanza wa Zanzibar Abeid Karume.* Watahiniwa walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu sherehe mbalimbali za kitaifa zinazoadhimishwa nchini Tanzania.


Hata hivyo, watahiniwa197,870 (19.53%) walivutiwa na kipotoshi B, *Ni siku ya kifo cha Rais wa kwanza wa Tanzania Julius K. Nyerere.* Watahiniwa waliochagua chaguo hili hawakuelewa kumbukumbu ya kifo cha Rais wa kwanza wa Tanzania ni tarehe 14 oktoba kila mwaka. Watahiniwa 172,638 (17.04%) walichagua kipotoshi C, *Ni siku ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar.* Chaguo hili pia halikuwa sahihi kwani muungano wa Tanganyika na Zanzibar huadhimishwa tarehe 26 Aprili kila mwaka. Vilevile, kipotoshi D, *Ni siku ya kuzaliwa TANU* kiliwavuta watahiniwa 132,070 (13.04%) ambao hawakufahamu kwamba chama cha TANU kilizaliwa tarehe 7 Julai 1954. Vilevile kipotoshi E, *Ni siku ya uhuru wa Zanzibar* kiliwavuta watahiniwa 53,272 (5.26%) ambao hawana ufahamu kuhusu historia ya Zanzibar. Watahiniwa hawa walipaswa kufahamu

kuwa sherehe ya uhuru kwa Zanzibar inaadhimishwa tarehe 12 Januari kila mwaka na siyo tarehe 7 Aprili.

**Swali la 6:** Ni vyombo gani vya kitamaduni hutumika kupikia chakula?

A Chungu na ngao
B Chungu na mwiko
C Ngao na kikapu
D Kinu na chungu
E Mtungi na kinu

Swali lilitoka katika mada ya *Utamaduni Wetu* na liliwataka watahiniwa kubaini majina ya vyombo vya kitamaduni ambavyo hutumika kupikia chakula. Ufaulu wa watahiniwa ulikuwa mzuri ambapo watahiniwa 815,483 (80.50%) waliweza kubaini jibu sahihi B, *Chungu na mwiko.* Watahiniwa wengi walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu vyombo mbalimbali vya kitamaduni vinavyotumika kupikia chakula. Chati Na. 4 inaonyesha ufaulu wa watahiniwa katika swali la 6.




**Chati Na. 4:** *Ufaulu mzuri wa watahiniwa katika swali la 6*

Kwa upande mwingine, watahiniwa 72,368 (7.14%) walichagua kipotoshi A*, Chungu na ngao.* Hawakufahamu kwamba ngao ni kifaa cha kitamaduni kinachotumika kujikinga na mashambulizi ya adui wakati wa vita vya ana kwa ana. Jumla ya watahiniwa 64,366 (6.35%) walivutiwa na kipotoshi D*, Kinu na chungu.* Kundi hili la watahiniwa lilishindwa kubaini kuwa kinu ni kifaa cha kitamaduni kinachotumika kukoboa na kusaga nafaka, kama vile mahindi au mpunga.


Watahiniwa 31,375 (3.10%) walichagua C, *Ngao na kikapu. Hawa* walishindwa kubaini kwamba ngao ni kifaa cha kitamaduni cha

kivita, na kikapu ni kifaa cha kitamaduni kinachotumika kuhifadhi na kubebea bidhaa mbalimbali kama vile nafaka na unga. Hata hivyo, watahiniwa 24,239 (2.39%) walivutiwa na kipotoshi E, *Mtungi na kinu* chaguo hili halikuwa sahihi kwa sababu mtungi ni chombo cha kitamaduni kinachotumika kuhifadhi maji au nafaka na kinu hutumika kukoboa au kusaga nafaka. Kwa ujumla, watahiniwa walioshindwa kubaini jibu sahihi hawakuwa na uelewa wa vyombo vya kitamaduni vinavyotumika kupikia chakula.

**Swali la 7:** Yupi kati ya wafuatao huendesha vikao vya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Spika na Naibu spika wanapokuwa hawapo Bungeni?

A Mwanasheria Mkuu wa Serikali
B Wenyeviti wa Bunge
C Waziri Mkuu
D Katibu wa Bunge
E Wenyeviti wa Kamati za Bunge

Swali lilitoka katika mada ya *Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania* na liliwataka watahiniwa kubaini kiongozi anayeendesha vikao vya bunge wakati Spika na Naibu Spika hawapo bungeni. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa hafifu ambapo watahiniwa 227,063 (22.41%) tu waliweza kubaini jibu sahihi B, *Wenyeviti wa Bunge.* Watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu viongozi wenye dhamana ya kuongoza vikao vya bunge endapo spika na naibu spika hawapo bungeni. Chati Na.5 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali la 7.




**Chati Na. 5:** *Ufaulu hafifu wa watahiniwa katika swali la 7*

Kwa upande mwingine, watahiniwa wengi 383,575 (37.86%) walivutiwa na kipotoshi C *Waziri Mkuu.* Watahiniwa waliochagua kipotoshi hiki walishindwa kutofautisha majukumu ya kiongozi wa shughuli za serikali bungeni na uongozi wa bunge hivyo kudhani kwamba huenda Waziri Mkuu anaweza pia kuongoza vikao vya bunge. Watahiniwa 204,704 (20.21%) walivutiwa na kipotoshi D, *Katibu wa Bunge.* Katibu wa Bunge huteuliwa na Raisi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ni kiongozi wa sekretarieti ya bunge na mshauri mkuu wa spika katika mambo yote ya utawala na uendeshaji wa bunge. Hivyo, hana jukumu la kuendesha vikao vya bunge.

Vilevile, watahiniwa 116,108 (11.46%) walivutiwa na kipotoshi A, *Mwanasheria Mkuu wa Serikali.* Watahiniwa waliochagua kipotoshi hiki hawakujua kuwa Mwanasheria Mkuu wa serikali ni mbunge kwa mujibu wa nafasi yake, na kazi yake kubwa ni kuishauri serikali katika mambo yote ya kisheria. Mwisho, watahiniwa 73,987 (7.30%) walivutiwa na kipotoshi E, *Wenyeviti wa Kamati za Bunge.* Watahiniwa waliovutiwa na kipotoshi hiki hawakujua kuwa kwa mujibu wa kanuni za uendeshaji bunge, majukumu ya wenyeviti wa kamati za Bunge ni kuongoza vikao vya kamati za bunge tu. Hivyo, hawana mamlaka ya kuongoza vikao vya bunge zima.

**Swali la 8:** Ipi kati ya zifuatazo ni faida ya kiuchumi ya kuwekeza katika elimu ya rasilimali watu Tanzania?

A Ufanisi katika kusimamia rasilimali za taifa.
B Uwepo wa sekta iliyo rasmi tu.
C Watu wote kupata kipato sawa.
D Kutoweka kwa utandawazi.
E Kupungua kwa bidhaa kutoka nchi za nje.

**Jedwali Na. 3: Idadi na asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo**

| Machaguo | A* | B | C | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 572,325 | 81,092 | 166,684 | 72,198 | 110,148 | 10,617 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 56,49 | 8.00 | 16.45 | 7.13 | 10.87 | 1.05 |

Swali hili lilitoka katika mada ya *Uchumi Wetu* na liliwataka watahiniwa kubaini faida za kiuchumi za kuwekeza katika elimu ya

rasimali watu nchini Tanzania. Kama inavyooneshwa katika Jedwali Na. 3, ufaulu katika swali hili ulikuwa wa wastani ambapo watahiniwa 572,325 (56.5%) waliweza kuchagua jibu sahihi A, *Ufanisi katika kusimamia rasilimali za taifa.* Watahiniwa walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu faida za kuwekeza katika elimu ya rasilimali watu. Rasilimali watu wenye elimu ya kutosha wanaweza kutumia elimu yao kumudu mazingira yanayowazunguka, kuleta tija katika uzalishaji mali na kuleta maisha bora kwa jamii nzima.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 166,684 (16.45%) walivutiwa na kipotoshi C, *Watu wote kupata kipato sawa.* Hawakufahamu kuwa uwekezaji katika elimu ya rasilimali watu hauwezi kuleta kipato sawa kutokana na mgawanyo wa kazi uliopo katika jamii. Watahiniwa 110,148 (10.87%) walichagua kipotoshi E, *Kupungua kwa bidhaa kutoka nchi za nje.* Watahiniwa waliochagua kipotoshi hiki waliamini uwekezaji katika elimu ya rasilimali watu ungeweza kupunguza uingizaji bidhaa kutoka nje jambo ambalo haliwezekani kutokana na ukweli kwamba hakuna nchi duniani inayojitosheleza kwa kila kitu. Aidha, watahiniwa 81,092 (8.00%) walivutiwa na kipotoshi B, *Uwepo wa sekta iliyo rasmi tu.* Kundi hili la watahiniwa halikufahamu kuwa kutokana na mazingira ya sasa ya uchumi wa soko huria na kushamiri kwa utandawazi ni vigumu kwa nchi kuwa na uchumi unaotegemea sekta moja tu iliyo rasmi. Mwisho, watahiniwa 72,198 (7.13%) walivutiwa na kipotoshi D, *Kutoweka kwa utandawazi.* Kundi hili la watahiniwa lilikosa ufahamu wa namna ambavyo utandawazi umeweza kushamiri. Hivyo, waliamini kimakosa kwamba uwekezaji katika elimu ya rasilimali watu ungeweza kusababisha utandawazi kutoweka. Ikumbukwe kuwa utandawazi umeshamiri kwa kiasi kikubwa kutokana na mapinduzi makubwa katika teknolojia ya habari na mawasiliano duniani.

**Swali la 9:** Upi kati ya ujumbe ufuatao hutolewa kwa madereva na watumiaji wengine wa barabara kwa kutumia rangi nyekundu katika taa za barabani?

A Ongeza mwendo
B Punguza mwendo
C Simama
D Kuna hatari mbele
E Kuna reli inapita mbele

**Jedwali Na. 4: Idadi na asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo**

| Machaguo | A | B | C* | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya watahiniwa | 37,493 | 185,176 | 559,073 | 199,860 | 24,352 | 7,110 |
| Asilimia ya watahiniwa | 3.70 | 18.28 | 55.19 | 19.73 | 2.40 | 0.70 |

Swali lilitoka katika mada ya *Ulinzi na Usalama* na liliwataka watahiniwa kubaini ujumbe unaotolewa kwa madereva na watumiaji wengine kupitia rangi nyekundu katika taa za barabarani. Kama inavyooneshwa katika Jedwali Na. 4, ufaulu katika swali hili ulikuwa wa wastani ambapo watahiniwa 559,073 (55.19%) waliweza kubaini jibu sahihi C, *Simama.* Watahiniwa hao walikuwa na ufahamu wa kutosha kuhusu alama mbalimbali za usalama barabarani.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 199,860 (19.73%) walivutiwa na kipotoshi D, *Kuna hatari mbele.* Watahiniwa waliochagua kipotoshi hiki walishindwa kutofautisha kati ya alama inayotoa tahadhari na alama inayotoa amri ya kusimama. Alama nyekundu katika taa za barabarani inatoa amri ya kusimama na siyo vinginevyo. Watahiniwa 185,176 (18.28%) walivutiwa na kipotoshi B, *Punguza mwendo.* Watahiniwa waliochagua kipotoshi hiki hawakujua kuwa kwa mujibu wa viwango vya kimataifa vya usalama barabarani rangi ya njano katika taa za barabarani zinatoa ujumbe wa kupunguza mwendo. Vilevile, watahiniwa 37,493 (3.70%) waliovutiwa na kipotoshi A, *Ongeza mwendo.* Walishindwa kuelewa kwamba ujumbe wa kuongeza mwendo au pita haraka hutolewa na taa za kijani. Mwisho, watahiniwa wachache 24,352 (2.40%) walichagua kipotoshi E, *Kuna reli inapita mbele.* Watahiniwa waliochagua kipotoshi hiki hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu alama za barabarani na ujumbe unatolewa na rangi nyekundu katika taa za barabarani kwani taarifa za uwepo wa reli sehemu yeyote ambapo reli inakutana na barabara huambatana na alama zingine za ziadi, sambamba na taa za rangi nyekundu kuruhusu au kuzuia magari wakati gari moshi linavuka barabara.

**Swali la 10:** Makao Makuu ya Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC) yapo katika mji gani?

A Pretoria B Lusaka C Harare
D Maputo E Gaboroni

**Jedwali Na. 5: Idadi na asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo**

| Machaguo | A | B | C | D | E* | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya watahiniwa | 89,870 | 219970 | 95,003 | 89,888 | 507,313 | 11,020 |
| Asilimia ya watahiniwa | 8.87 | 21.71 | 9.38 | 8.87 | 50.08 | 1.09 |

Swali lilitungwa kutoka katika mada ya *Ushirikiano wa Tanzania na Mataifa mengine,* na liliwataka watahiniwa kubaini jina la mji ambao ni makao makuu ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC). Kama ilivyooneshwa katika Jedwali 5, ufaulu katika swali hili ulikuwa wa wastani ambapo watahiniwa 507,313 (50.08%) waliweza kubaini jibu sahihi E, *Gaboroni.* Kwa ujumla, watahiniwa walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu jumuiya za kiuchumi zilizopo Afrika na miji ambayo ni makao makuu ya jumuiya hizo.


Kwa upande mwingine, watahiniwa walichagua machaguo yasiyo sahihi kama ifuatavyo: Watahiniwa wengi 219,970 (21.71%) walichagua B, Lusaka kwa sababu wazo la kuunda SADCC lilizaliwa Lusaka kupitia tamko la Lusaka tarehe 1 April 1980. Ilipofika mwaka 1992, SADCC ilibadilishwa na kuwa SADC; watahiniwa walishindwa kuhusianisha sehemu iliyozaa wazo la kuunda SADCC na makao makuu ya sasa ya Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC). Vilevile, chaguo A, *Pretoria,* (mji mkuu wa Afrika ya Kusini) ulivutia watahiniwa 89, 870 (8.87%); chaguo C, *Harare* (mji mkuu wa Zimbabwe) ulivutia watahiniwa 95,003 (9.38 %) na chaguo D, *Maputo* (mji mkuu wa msumbiji) ulivutia watahiniwa 89,888 (8.87%). Kuna mwelekeo wa idadi na asilimia ya watahiniwa ambayo tunaweza kubaini kwa machaguo A, C na D. Idadi na asilimia ya watahiniwa waliochagua vipotoshi hivi inakaribiana sana kwa kila chaguo. Mwelekeo huo unatoa taswira kuwa vipotoshi hivyo vilivutia watahiniwa kwa uwiano sawa.

**Swali la 11:** Yupi kati ya wanyama wafuatao anaweza kulinda maisha na mali zetu?

A Farasi B Punda C Ngamia
D Paka E Mbwa

Swali lilitoka katika mada ya *Ulinzi na Usalama katika ngazi ya familia,* na liliwataka watahiniwa kubaini jina la mnyama ambaye

anaweza kulinda maisha ya binadamu na mali zake. Ufaulu katika swali hili ulikuwa mzuri ambapo watahiniwa 896,344 (88.48%) waliweza kubaini jibu sahihi E, *Mbwa.* Watahiniwa wengi walikuwa na ufahamu wa mnyama anayetumika katika nyumba nyingi kulinda maisha na mali za watu. Hivyo, ilikuwa rahisi kwa watahiniwa kuhaulisha uzoefu wa maisha yao ya kila siku kujibu swali hili. Chati Na. 6 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali la 11.





**Chati Na. 6:** *Ufaulu mzuri wa watahiniwa katika swali la 11*

Kwa upande mwingine, watahiniwa 25,057 (2.47%) walichagua kipotoshi A, *Farasi*, bila kujua ukweli kuwa farasi ni mnyama ambaye hutumika kama njia ya asili ya usafiri tangu siku nyingi. Vilevile, watahiniwa 24,905 (2.46%) walichagua B, *Punda.* Watahiniwa hao hawakufahamu kuwa punda anatumika katika jamii nyingi kusafirisha mizigo. Pia watahiniwa 31,128 (3.07%) walichagua C, *Ngamia* hawakujua kuwa kwa sababu za kibayolojia, ngamia anatumika kusafirisha watu na mizigo katika maeneo ya jangwa. Mwisho, watahiniwa 28,248 (2.79%) walichagua D, *Paka,* kwa sababu katika jamii nyingi paka ni mnyama anayefugwa nyumbani na hutumika kudhibiti panya.

**Swali la 12:** Ni kwa namna gani Tanzania inaweza kunufaika na utandawazi?

A Kuwa na uwezo wa kupanga bei za bidhaa zake katika soko la kimataifa.
B Kupata fursa ya kuwekeza katika nchi tajiri duniani.
C Kuwa na uwezo wa kuwa na kura ya turufu katika Umoja wa Mataifa.
D Kupata fursa ya kutangaza vivutio vyake vya utalii.
E Vijana wengi kupata fursa za ajira katika nchi tajiri.

Swali lilitoka katika mada ya *Utamaduni wa Tanzania na Tamaduni nyingine,* na liliwataka watahiniwa kubaini manufaa yanayoweza kupatikana kwa Tanzania kupitia utandawazi. Jedwali la 6 linaonesha ufaulu wa watahiniwa kuwa ni hafifu ambapo watahiniwa wachache 358,653 (35.40%) waliweza kuchagua jibu sahihi D, *Kupata fursa ya kutangaza vivutio vyake vya utalii.* Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu manufaa yatokanayo na utandawazi. Utandawazi huchochewa pamoja na mambo mengine na usafirishaji wa mitaji duniani, mapinduzi katika teknolojia ya habari na mawasiliano ambayo yanahamasisha watu kusafiri duniani kote bila kipingamizi. Kutokana na hali hiyo, Tanzania inaweza kutumia fursa hiyo kutangaza vivutio vyake vya utalii na kuhamasisha watalii kutembelea Tanzania. Chati Na.7 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali la 12.




**Chati Na. 7**: *Ufaulu hafifu wa watahiniwa katika swali la 12*

Kwa upande mwingine, watahiniwa 297,371 (29.35%) walichagua A, *Kuwa na uwezo wa kupanga bei za bidhaa zake katika soko la kimataifa. Watahiniwa hao* hawakujua kuwa soko la sasa la kimataifa limetawaliwa na nchi tajiri za magharibi. Chaguo B, *Kupata fursa ya kuwekeza katika nchi tajiri duniani,* halikuwa jibu sahihi kwa sababu tofauti kati ya nchi tajiri na nchi masikini hazitoi fursa kwa nchi kama Tanzania kuwekeza katika nchi tajiri za viwanda. Vilevile, watahiniwa 120,340 (11.88%) walichagua kipotoshi C, *Kuwa na uwezo wa kuwa na kura ya turufu katika Umoja wa Mataifa.* Hawakuwa na ufahamu wa chata ya Umoja wa Mataifa. Chata ya Umoja wa mataifa inatoa upendeleo wa kura ya turufu kwa wanachama watano wa kudumu wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa. Mwisho, watahiniwa 82,596 (8.15%) walivutiwa na chaguo E, *Vijana wengi kupata fursa za ajira katika nchi tajiri.* Watahiniwa hawakujua kuwa maendeleo ya teknolojia hayatengenezi ajira kwa watu walio wengi. Kazi nyingi zinafanywa na mashine kupunguza gharama za nguvu kazi. Kutokana na hali hiyo, kuna fursa za ajira katika nchi zinazoendelea kwani kazi nyingi zinahitaji matumizi ya nguvu kazi zaidi kuliko katika nchi tajiri ambapo kazi nyingi kutokana na maendeleo ya kiteknolojia zinahitaji watu wachache.

### 2.1.2. Kipengele II: Historia

**Swali la 13:** Ni nani aliyegundua moto katika Zama za Kati za Mawe?

A Primeti
B Homo Habilisi
C Homo Erectus
D Australopithikasi
E Homo Sapiensi

**Jedwali Na. 6: Idadi na asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo**

| Machaguo | A | B | C* | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 440,055 | 340,352 | 245,571 | 105,427 | 267,714 | 9,945 |
| **Asilimia ya Watahiniwa** | 4.30 | 33.60 | 24.20 | 10.40 | 26.40 | 1.00 |

Swali lilitungwa kutoka katika mada ya *Chimbuko na Mabadiliko ya Binadamu*. Swali liliwataka watahiniwa kubaini jina la mwanadamu wa mwanzo aliyegundua moto katika Zama za Kati za Mawe. Ufaulu katika swali hili ulikuwa dhaifu kwani watahiniwa 245,571 (24.20%) tu ndio walioweza kuchagua jibu sahihi C, *Homo Erectus*. Watahiniwa hao, walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mabadiliko ya kimaumbile ya binadamu, maendeleo ya teknolojia yaliyokuwa yameshafikiwa katika kila hatua na vipindi ambavyo hatua hizo za kimaendeleo au kiteknolojia zilifikiwa.

Hata hivyo, jumla ya watahiniwa 767,493 (75.80%) walichagua vipotoshi: A, *Primeti*; B, *Homo Habilis;* D, *Australopithikasi* na E, *Homo Sapiens.* Uchaguzi wa vipotoshi hivyo unaashiria kuwa watahiniwa wengi hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mabadiliko ya umbile la binadamu, sifa na hatua za uvumbuzi zilizokuwa zimeshafanywa katika kila zama.

**Swali la 14:** Vipi vilikuwa vyama maarufu vya siasa vilivyopigania uhuru wa Zimbabwe?

A KANU na UNIP  B UNITA na ZANU
C ZANU na MPLA  D ZNP na ZANU
E ZAPU na ZANU

**Jedwali Na. 7: Idadi na asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo**

| Machaguo | A | B | C | D | E* | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahinwa | 135,112 | 124,701 | 260,032 | 228,161 | 256,888 | 8,170 |
| Asilimia ya Watahiniwa | 13.30 | 12.30 | 25.70 | 22.50 | 25.40 | 0.80 |


Swali lilitungwa kutoka katika mada ya *Harakati za Kupigania Uhuru katika Afrika*. Swali lilipima uwezo wa watahiniwa kubaini majina ya vyama vya siasa vilivyopigania uhuru wa Zimbabwe. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa ni hafifu kwani watahiniwa 256,888 (25.40%) tu ndio waliweza kuchagua jibu sahihi E, *ZAPU* na *ZANU*. Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu vyama vya siasa vilivyopigania uhuru katika nchi husika katika Afrika.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 756,176 (74.60%) walichagua machaguo yasiyo sahihi. Watahiniwa hao walipaswa kuelewa kuwa KANU, UNIP, UNITA na MPLA na ZNP vilikuwa vyama vya siasa vilivyopigania uhuru wa Kenya, Zambia, Angola na Zanzibar mtawalia. Hivyo, havikuhusika na kupigania uhuru wa Zimbabwe.

**Swali la 15:** Ni jamii ipi ilipinga uvamizi wa Kiingereza kwa njia ya vita katika Afrika ya Kati?

A Wamatumbi B Wamandika C Wakhoisa
D Wandebele E Waasante

Swali hili lilitungwa kutoka katika mada ya *Uvamizi wa Kikoloni katika Afrika kuanzia mwaka 1880* na liliwataka watahiniwa kubaini jina la jamii iliyopinga uvamizi wa Kiingereza kwa njia ya vita katika Afrika ya Kati. Kwa ujumla, kiwango cha ufaulu cha watahiniwa katika swali hili kilikuwa cha wastani kama inavyoonekana kwenye. Chati Na. 8.




**Chati Na. 8:** *Ufaulu wa wastani wa watahiniwa katika swali la 15*

Jumla ya watahiniwa 468,076 (46.20%) walichagua jibu sahihi D, *Wandebele.* Watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu mahali na jina la jamii ya Kiafrika iliyopinga uvamizi wa kikoloni kwa njia ya vita katika karne ya 19 mwishoni na mwanzoni mwa karne ya 20.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 215,209 (21.24%) walichagua kipotoshi A, *Wamatumbi.* Watahiniwa hao hawakuwa na maarifa kuhusu jamii za Kiafrika na mbinu walizotumia kupinga uvamizi wa kikoloni. Watahiniwa hao walishindwa kuelewa kuwa Wamatumbi

kwa kushirikiana na makabila mengine walipigana vita vya Majimaji Kusini mwa Tanganyika (kwa sasa Tanzania) dhidi ya Wajerumani na siyo Afrika ya kati dhidi ya Waingereza.

Pamoja na hayo, watahiniwa 123,142 (12.16%) walichagua kipotoshi B, *Wamandika.* Uchaguzi wa kipotoshi hicho unathibitisha kuwa watahiniwa hao walikuwa na uelewa mdogo kuhusu upinzani dhidi ya uvamizi wa kikoloni katika Afrika. Watahiniwa hao hawakujua kwamba Wamandika sio jamii ya Afrika ya Kati bali ni jamii ya Afrika Magharibi iliyopinga uvamizi wa Wafaransa Afrika ya Magharibi chini ya uongozi wa Samori Toure na sio uvamizi wa Waingereza katika Afrika ya Kati.

Vilevile, jumla ya watahiniwa 92,942 (9.17%) walichagua kipotoshi C, *Wakhoisa* ilhali kipotoshi E, *Asante,* kiliwavutia 106,365 (10.50%). Watahiniwa hao, walishindwa kutambua jamii sahihi na mahali ambapo upinzani dhidi ya uvamizi wa wakoloni ulitokea. Watahiniwa hao walipaswa kuelewa kwamba jamii ya Wakhoisa walipinga uvamizi wa Waingeza katika Afrika Kusini na Waasante walipinga uvamizi wa Wadachi Afrika Magharibi na sio Afrika ya Kati.

**Swali la 16:** Ni taifa gani la Ulaya lililosaini makubaliano ya Buganda yaliyompa kabaka madaraka ya kisiasa mwaka 1900?

A Ubelgiji
B Marekani
C Ujerumani
D Ufaransa
E Uingereza

**Jedwali Na. 8: Idadi na asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo**

| Machaguo | A | B | C | D | E* | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 193,414 | 105,599 | 221,446 | 135,717 | 348,072 | 8,816 |
| Asilimia ya Watahiniwa | 19.10 | 10.40 | 21.90 | 13.40 | 34.40 | 0.90 |

Swali hili lilitoka katika mada ya *Kuanzishwa kwa Utawala wa Kikoloni katika Afrika.* Swali liliwataka watahiniwa kubaini jina la taifa la Ulaya lililosaini makubaliano ya Buganda yaliyompa Kabaka madaraka ya kisiasa mwaka 1900. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa dhaifu kwani ni watahiniwa 348,072 (34.40%) tu waliochagua jibu sahihi E, *Uingereza.* Watahiniwa hao walikuwa na

maarifa kuwa makubaliano ya Buganda yalileta utengano Uganda kutokana na Waingereza kutumia mbinu ya kugawa watu na kuwatawala. Makubaliano ya Buganda yalimpa Kabaka, familia ya Kifalme na Katikiro (watawala) upendeleo wa kipekee na kufanya watawala wa Buganda kuwa watiifu kwa ukoloni wa Kiingereza.

Jumla ya watahiniwa 193,414 (19.10%) walichagua kipotoshi A, *Ubelgiji*. Chaguo hilo halikuwa sahihi kwa sababu Ubelgiji ilitawala Zaire, inayojulikana kwa sasa kama Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo (DRC) na sio Uganda.

Kipotoshi B, Marekani kilichaguliwa na watahiniwa 105,599 (10.40%). Chaguo hilo halikuwa sahihi kwa sababu Marekani sio nchi ya Ulaya, vilevile haikushiriki kugombania, kugawana wala kuitawala Afrika.

Vilevile, watahiniwa 221,446 (21.90%) walichagua kipotoshi C, *Ujerumani.* Chaguo hilo halikuwa sahihi kwa sababu ukoloni wa Wajerumani katika Afrika Magharibi ulijikita katika koloni la Ujerumani la Afrika Mashariki (Tanganyika) na sio Uganda ambapo palikuwa na Dola ya Buganda.

Pia, watahiniwa 135,717 (13.40%) walichagua kipotoshi D, *Ufaransa*. Uchaguzi wa kipotoshi hicho ulisababishwa na uelewa mdogo wa watahiniwa kuhusu mataifa ya Ulaya yaliyogombania na kugawana bara la Afrika miongoni mwao. Watahiniwa hawa walishindwa kuelewa kwamba Ufaransa haikugombania wala kutawala nchi yoyote Afrika Mshariki bali ilielekeza nguvu zake katika kutawala nchi za Afrika Magharibi.

**Swali la 17:** Ni nchi gani mfumo wa kulisha kasumba ulianzishwa kwa mara ya kwanza?

A Naijeria  B Msumbiji
C Uganda  D Angola
E Senegali

Swali hili lilitoka katika mada ya *Kuanzishwa kwa Utawala wa Kikoloni katika Afrika*. Swali liliwataka watahiniwa kubaini jina la nchi ambayo mfumo wa kulisha kasumba ulianzishwa kwa mara ya kwanza. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa wa kiwango dhaifu kwa sababu watahiniwa 272,074 (26.86%) tu ndio


waliochagua jibu sahihi E, *Senegali*. Watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu mbinu na sera walizotumia wakoloni kutawala makoloni Afrika. Walifahamu kuwa mfumo wa utawala wa kulisha kasumba ulianzishwa na Wafaransa kwa mara ya kwanza nchini Senegali. Wafaransa walianzisha mfumo huo baada ya mapinduzi ya Ufaransa yaliyotokea mwaka 1789 hadi1799. Katika mapinduzi hayo, wanamapinduzi walisisitiza usawa na kuthamini utu wa binadamu.

Kipotoshi B, *Msumbiji* kiliwavutia watahiniwa 243,258 (24.01%). Watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa kutosha kuwa mfumo wa utawala wa kulisha kasumba ulianzishwa Msumbiji na Wareno lakini hawakuelewa kuwa ulianzishwa kwa mara ya kwanza na Wafaransa nchini Senegali.

Kipotoshi kingine kilichowavutia watahiniwa wengi (199,062, sawa na asilimia 19.60) ni D, *Angola.* Chaguo hilo halikuwa sahihi kwa sababu Angola haikuwa nchi ya kwanza ambako mfumo wa kulisha kasumba ulianzishwa.

Kipotoshi A, *Naijeria,* kilichaguliwa na watahiniwa 267,091 (16.49%). Hili halikuwa jibu sahihi kwa sababu mfumo wa utawala wa kulisha kasumba haukutumika Naijeria. Naijeria ilikuwa nchi ya kwanza ambako mfumo wa utawala wa mlango wa nyuma ulianzishwa na Waingereza chini ya Kapteni Fredrick Lugard mwaka 1914.

Jumla ya watahiniwa 120,511 (11.90%) walichagua kipotoshi C, *Uganda*. Hilo halikuwa jibu sahihi kwa sababu mfumo wa utawala wa kulisha kasumba haukutumika nchini Uganda. Uganda ilitawaliwa na Waingereza waliokuwa wakitumia mfumo wa utawala wa mlango wa nyuma. Kwa ujumla, tunachojifunza kutokana na machaguo hayo yasiyo sahihi yanatokana na watahiniwa hao kutokuwa na ufahamu wa kutosha kuhusu mifumo ya tawala za ukoloni iliyotumiwa katika kuendesha shughuli za kiutawala kwenye makoloni yao katika Afrika. Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 17 umeoneshwa katika Chati Na. 9.




**Chati Na. 9:** *Ufaulu hafifu wa watahiniwa katika swali la 17*

**Swali la 18:** Ni karne ya ngapi mataifa ya Ulaya yalilivamia Bara la Afrika?

A Karne ya 15
B Karne ya 20
C Karne ya 18
D Karne ya 9
E Karne ya 19

**Jedwali Na. 9: Idadi na asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo**

| Machaguo | A | B | C | D | E* | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 297,429 | 77,509 | 198,255 | 140,809 | 290,339 | 8,723 |
| Asilimia ya Watahiniwa | 29.40 | 7.70 | 19.60 | 13.90 | 28.70 | 0.90 |

Swali hili lilitoka katika mada ya *Kuvamiwa kwa Bara la Afrika.* Swali liliwataka watahiniwa kubaini karne ambapo mataifa ya Ulaya yalilivamia Bara la Afrika. Kiwango cha ufaulu kwa ujumla kilikuwa hafifu kwani watahiniwa 722,725 (71.30%) walichagua vipotoshi A, *Karne ya 15;* B, *Karne ya 20*; C *Karne ya 18* na D, *Karne ya 9*. Uchaguzi wa vipotoshi hivi unaonesha kuwa watahiniwa hao hawakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu karne ambayo mataifa ya Ulaya yalilivamia Bara la Afrika. Kwa ujumla, watahiniwa hao, walipaswa kuelewa kuwa katika karne ya 15 ni kipindi ambapo mataifa ya Ulaya (Wareno) walikuwa na uhusiano wa kibiashara na jamii za Afrika. Vilevile, karne ya 20 ndicho kipindi ambacho nchi

nyingi za Afrika zilipata uhuru wake na karne ya 18 kulitokea mageuzi ya viwanda katika baadhi ya nchi huko Ulaya. Pamoja na hayo, karne ya 9 ni kipindi ambacho jamii za Waasia walikuwa na uhusiano wa kibiashara na jamii za Afrika Mashariki. Kwa ufupi, watahiniwa katika kundi hii hawakuwa na uelewa wa matukio ya kihistoria na muda ambayo matukio hayo yalitokea.

Jumla ya watahiniwa 290,339 (28.70%) walichagua jibu sahihi E, *Karne ya 19.* Watahiwa hao, walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu uvamizi mkubwa wa Bara la Afrika ulofanywa na mataifa ya kibepari kutoka Ulaya mara tu baada ya mapinduzi ya viwanda huko Ulaya.

**Swali la 19:** Nani alikuwa binadamu wa kwanza kutengeneza zana na ambaye alikuwa na ubongo mkubwa kuliko wa Zinjanthropasi?

| | | | |
|---|---|---|---|
| A | Homo Erectus | B | Homo Sapiens |
| C | Homo Habilisi | D | Australopithikasi |
| E | Primeti | | |


Swali lilitoka katika mada ya *Chimbuko na Mabadiliko ya Binadamu.* Swali liliwataka watahiniwa kubaini jina la binadamu wa kwanza kutengeneza zana na ambaye alikuwa na ubongo mkubwa kuliko wa Zinjanthropasi. Ufaulu katika swali hili ulikuwa dhaifu kwani ni watahiniwa 299,805 (29.50%) tu waliweza kuchagua jibu sahihi C, *Homo Habilisi.* Watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu Chimbuko na Mabadiliko ya Binadamu na maendeleo ya kiteknolojia yaliyokuwa yamefikiwa na mwanadamu wa mwanzo katika kila hatua ya mabadiliko ya binadamu.

Hata hivyo, watahiniwa 315,159 (31.10%) walichagua kipotoshi B, *Homo Sapiens*. Watahiniwa hawa walipaswa kuelewa kuwa Homo Sapiens hakuwa binadamu wa kwanza kutengeneza zana bali aliboresha zana na silaha zilizotengenezwa na Homo Erectus. Homo Sapiens alikuwa binadamu wa kwanza kuchora mapangoni na kujihusisha na ufugaji.

Vile vile, watahiniwa 184,570 (18.20%) walichagua kipotoshi A, *Homo Erectus*. Uchaguzi wa kipotoshi hiki ulisababishwa na uelewa mdogo wa watahiniwa kuhusu hatua za maendeleo ya binadamu katika zama mbalimbali. Watahiniwa hawa walishindwa kuelewa

kwamba Homo Erectus hakuwa binadamu wa kwanza kutengeneza zana bali aliboresha zana (kama vile shoka na mikuki) zaidi ya zile za Homo Habilisi. Homo Erectus alikuwa binadamu wa kwanza kugundua moto na kutembea wima.

Kipotoshi E, *Primeti,* kilichaguliwa na watahiniwa 59,471 (5.87%) na wengine 143,312 (14.15%) walichagua kipotoshi D *Australopithikasi*. Watahiniwa hawa walikosa maarifa ya kutosha kuhusu mabadiliko ya umbile la binadamu katika nyakati mbalimbali. Watahiniwa katika kundi hili walipaswa kuelewa kwamba Primeti na Australopithikasi walikuwa katika hatua za mwanzo za mabadiliko ya umbile la binadamu. Katika hatua hizo za mwanzo, umbile la binadamu lilifanana sana na lile la sokwe ambaye aliishi msituni kama wanyama wengine na kula wadudu, mayai ya ndege na majani. Hatua kubwa aliyofikia binadamu katika kipindi hicho ni kutembea kwa miguu miwili. Hivyo, sio sahihi kuhusianisha Primeti na Australopithikasi na utengenezaji wa zana. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili umeoneshwa katika Chati Na. 10.




**Chati Na. 10**: *Ufaulu hafifu waa watahiniwa katika swali la 19*

**Swali la 20:** Ni katika zama gani mwanadamu alianza kuzalisha chakula zaidi?

A Zama za Mwisho za Mawe
B Zama za Mwanzo za Mawe
C Zama za Kati za Mawe
D Zama za Kale za Mawe
E Miaka milioni 30 kabla ya Kristo

**Jedwali Na. 10: Idadi na asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo**

| Machaguo | A* | B | C | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya Watahiniwa** | 617,272 | 54,675 | 244,797 | 35,950 | 53,211 | 7,159 |
| **Asilimia ya Watahiniwa** | 60.90 | 5.40 | 24.20 | 3.50 | 5.30 | 0.70 |

Swali hili lilitoka katika mada ya *Hatua za Maendeleo ya Binadamu Katika Zama Mbalimbali*. Swali liliwataka watahiniwa kubaini jina la zama ambayo mwanadamu alianza kuzalisha chakula zaidi. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa mzuri kwani watahiniwa 617,272 (60.90%) walichagua jibu sahihi A, *Zama za Mwisho za Mawe.* Watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu hatua za maendeleo ya binadamu katika zama mbalimbali. Aidha, waliewa kuwa uzalishaji wa chakula ulimwezesha binadamu kuwa na makazi ya kudumu, kuongezeka, kuboresha zana zake na na kuwa na mgawanyo wa kazi. Kwa jumla, uzalishaji zaidi wa chakula ulimwezesha binadamu kuyatawala mazingira yake.

Jumla ya watahiniwa 244,797 (24.20%) walivutiwa na kipotoshi C, *Zama za Kati za Mawe*. Kipotoshi hiki kiliwavutia watahiniwa wengi kwa sababu ya umaarufu wa kipindi hicho. Katika Zama za Mawe za Kati, binadamu aliweza kugundua moto. Hivyo, watahiniwa hao, walihusianisha ugunduzi wa moto na uzalishaji wa chakula. Pamoja na hayo, watahiniwa hao walishindwa kubaini shughuli halisi za kijamii, kiuchumi na kiteknolojia alizozifanya binadamu katika Zama mbalimbali za Mawe.

Watahiniwa waliochagua kipotoshi B, *Zama za Mwanzo za Mawe* na D, *Zama za Kale za Mawe* hawakuwa na ufahamu wa maendeleo ya kiuchumi na kiteknolojia katika zama hizo. Watahiniwa hao, walipaswa kufahamu kwamba *Zama za Mwanzo za Mawe* na *Zama za Kale za Mawe* zinatumika sawia kufafanua kipindi cha miaka kuanzia 1,750,000 KK hadi 750,000 KK. Vilevile, katika kipindi hiki binadamu aliweza kutengeneza zana za kuchimbia na kukatia. Hivyo, uchaguzi wa vipotoshi hivyo unathibitisha kuwa watahiniwa hawakuwa na maarifa ya kutosha ya mafanikio ya binadamu katika zama za mawe.

Vile vile, jumla ya watahiniwa 53,211 (5.30%) walichagua kipotoshi E, *Miaka milioni 30 kabla ya Kristo.* Watahiniwa hao, walishindwa kuelewa kwamba miaka milioni 30 kabla ya Kristo ni kipindi ambacho Primeti (Chimpanzi) aliishi. Hiki kilikuwa kipindi cha zama za mwanzo ambapo binadamu aliishi kwa kuwinda, kukusanya matunda na mizizi ya miti na kutembea kwa miguu minne. Kwa ujumla, watahiniwa waliochagua kipotoshi hiki hawakuwa na uelewa kuhusu muda, tabia na mpangilio wa hatua za mabadiliko ya binadamu pamoja na mafanikio yake kijamii, kiuchumi na kiteknolojia katika vipindi mbalimbali.

**Swali la 21:** Ni yupi kati ya wafuatao ni Katibu wa kamati ya shule?

A Mwalimu wa somo
B Mwalimu wa nidhamu
C Mtendaji wa kijiji
D Mwenyekiti wa kijiji
E Mwalimu Mkuu

**Jedwali 11: Idadi na wastani wa watahiniwa katika kila chaguo**

| Machaguo | A | B | C | D | E* | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya Watahiniwa** | **31,899** | **100,584** | **92,070** | **92,326** | **686,971** | **9,214** |
| **Asilimia ya Watahiniwa** | 3.10 | 9.90 | 9.10 | 9.10 | 67.80 | 0.90 |

Swali lilitoka katika mada ya *Shule Yetu* na liliwataka watahiniwa kubaini Katibu wa kamati ya shule kutoka kwenye machaguo waliyopewa. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri kwani watahiniwa 686,971 (67.80%) walichagua jibu sahihi E, *Mwalimu Mkuu.* Watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu uongozi katika ngazi ya shule.

Katika vipotoshi vyote, kipotoshi B, *Mwalimu wa nidhamu* kiliongoza kwa kuvutia watahiniwa 100,584 (9.90%). Kipotoshi hiki kilichaguliwa na wahiniwa pengine kwa sababu ya majukumu makubwa afanyayo mwalimu wa nidhamu shuleni katika kutatua masuala ya nidhamu ya wanafunzi. Kamati ya nidhamu chini ya ukatibu wa mwalimu wa nidhamu hukutana mara kwa mara ilihali kamati ya shule chini ya ukatibu wa mwalimu mkuu wa shule hukutana mara chache. Hivyo, watahiniwa walishindwa kuelewa utaratibu huo.

Vipotoshi C, *Mtendaji wa kijiji* na D, *Mwenyekiti wa kijiji* vilichaguliwa na watahiniwa waliokuwa na uelewa mdogo kuhusu uongozi katika ngazi ya shule.

**Swali la 22:** Ni lini mabaharia wa mwanzo wa Kireno walifika katika rasi ya Tumaini Jema?

A Karne ya 16 B Karne ya 18 C Karne ya 15
D Karne ya 12 E Karne ya 19

Swali hili lilitoka katika mada ya *Uhusiano wa Jamii za Kitanzania na Jamii nyingine za Kiasia na Kizungu.* Swali liliwataka watahiniwa kubaini karne ambapo mabaharia wa mwanzo wa Kireno walifika katika rasi ya Tumaini Jema. Kwa ujumla, ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa wa wastani kwani watahiniwa 467,494 (46.10%) walichagua jibu sahihi ni C, *Karne ya 15*. Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu uhusiano kati ya jamii za Afrika na jamii za Kizungu (Ulaya). Hivyo, waliweza kutambua kuwa mabaharia wa mwanzo wa Kireno walifika katika rasi ya Tumaini Jema chini ya uongozi wa Bartholomew Diaz katika karne ya 15 (1488).

Kipotoshi B, *Karne ya 18* kiliwavutia watahiniwa 180,886 (17.90%) wenye ufahamu hafifu kuhusu matukio ya kihistoria na wakati wake. Watahiniwa hao walipaswa kuelewa kuwa, katika karne 18, mabaharia wa mwanzo wa Kireno walishafika katika rasi ya Tumaini Jema kwa muda wa kipindi cha karne nne nyuma. Kwa ufupi, katika karne ya 18 kulitokea mapinduzi ya viwanda huko Ulaya na hayakuwa na uhusiano wa kuja kwa mabaharia wa mwanzo wa Kireno katika rasi ya Tumaini Jema.

Vilevile, jumla ya watahiniwa 172,627 (17.00%) walichagua kipotoshi E, *Karne ya 19*. Uchaguzi wa chaguo hili lisilo sahihi ulisababishwa na uwepo wa matukio mengi ya kihistoria yaliyohusisha Afrika na Ulaya. Matukio hayo ya kihistoria ni pamoja na kuja kwa vitangulizi vya ukoloni, kukomeshwa kwa biashara ya watumwa, mabeberu kugombania na kugawana bara la Afrika, kutawaliwa kwa bara la Afrika na upinzani wa Waafrika dhidi ya uvamizi wa kikoloni. Mvuto wa matukio haya ya kihistoria uliwavuti watahiniwa waliokuwa na ufahamu mdogo kuhusu uhusiano wa mwanzo kati ya Afrika na Ulaya, hivyo kuchagua jibu lisilo sahihi.

Hali kadhalika, vipotoshi A, *Karne ya 16,* kilichovutia watahiniwa 96,258 (9.50%) na D, *Karne ya 12,* kilichovutia jumla ya watahiniwa 86,965 (8.60%), havikuwa karne sahihi. Kwa ufupi, uchaguzi wa vipotoshi hivyo unaonesha kuwa watahiniwa hao hawakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu mwingiliano kati ya jamii ya Waafrika, Waasia na Wazungu na madhara yaliyotokana na mwingiliano huo kwa jamii za Kiafrika.


**Swali la 23:** Nchi zipi ni wajumbe wa kudumu wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa?

A China, Marekani, Ufaransa na Ujerumani
B China, Marekani, Ufaransa na Uingereza
C China, Marekani, Uingereza na Canada
D Uingereza, Ufaransa, Ujerumani na Marekani
E Uingereza, China, Ujerumani na Marekani

Swali lilitoka katika mada ya *Ushirikiano wa Kimataifa.* Swali liliwataka watahiniwa kubani majina ya nchi wanachama wa kudumu wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa. Ufaulu katika swali hili ulikuwa wa wastani kwani watahiniwa 306,929 (30.10%) waliweza kuchagua jibu sahihi B, *China, Marekani, Ufaransa na Uingereza.* Watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu mashirika ya Kimataifa na umuhimu wake.

Zaidi ya robo ya watahiniwa, sawa na asilimia 57.30%, walichagua vipotoshi A, *China, Marekani, Ufaransa na Ujeruman; D, Uingereza, Ufaransa, Ujerumani na Marekani* na E, *Uingereza, China, Ujerumani na Marekani*. Uchaguzi wa vipotoshi hivyo unaonesha kuwa watahiniwa hao walikuwa na uelewa mdogo kuhusu mada ya Ushirikiano wa Kimataifa. Watahiniwa hao walipaswa kuelewa kuwa Ujerumani siyo mjumbe wa kudumu wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa. Hivyo, machaguo hayo (A, D na E) hayakuwa sahihi.

Watahiniwa wengine (117,012, sawa na asilimia 11.6) walichagua kipotoshi C, *China, Marekani, Uingereza na Canada*. Jibu hili halikuwa sahihi kwa sababu Canada sio mjumbe wa kudumu wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa. Kwa ujumla, watahiniwa wengi walichagua machaguo yasiyokuwa sahihi kwa kuwa hawakuelewa muundo wa Baraza la Usalama wa Umoja wa Mataifa (UNO). Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 23 umeoneshwa katika Chati Na. 11.




**Chati Na. 11**: *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 23*

**Swali la 24:** Ni lini Jumuiya ya Madola ilianzishwa?

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| A | 1945 | B | 1921 | C | 1955 |
| D | 1919 | E | 1931 | | |

Swali liliwataka watahiniwa kubaini mwaka ambao Jumuia ya Madola ilianzishwa. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa hafifu kwani asilimia 71.40 ya watahiniwa walishindwa kuchagua jibu sahihi.

Zaidi ya robo ya watahiniwa (350,090 sawa na asilimia 34.60%) walichagua kipotoshi A, *1945.* Hili halikuwa jibu sahihi kwa sababu Jumuiya ya Madola haikuanzishwa mwaka 1945. Jumuiya ya Kimataifa ilyoanzishwa mwaka 1945 ni Umoja wa Mataifa (UNO). Kutokana na uchaguzi wa kipotoshi hiki, inaweza kuhitimishwa kwamba watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu muda na matukio ya kihistoria yaliyotokea katika karne ya 20.

Kipotoshi D, *1919* kilichaguliwa na watahini 137,998 (13.60%). Watahiniwa hao walishindwa kuelewa kwamba mwaka 1919 ni kipindi ambacho Uingereza walianza rasmi kuitawala Tanganyika na sio kipindi ambacho Jumuiya ya Madola ilianzishwa.

Aidha, jumla ya watahiniwa 135,704 (13.40%) walichagua kipotoshi C, *1955.* Hilo halikuwa jibu sahihi kwani Jumuiya ya Kimataifa iliyoanzishwa mwaka 1955 ni Jumuiya ya Nchi Zisizofungamana na Upande Wowote (Non Aligned Movement - NAM) na sio Jumuia ya Madola.

Vilevile, jumla ya watahiniwa 88,592 (8.70%) walichagua kipotoshi B, *1921.* Hilo halikuwa chaguo sahihi kwani mwaka huo hauna uhusiano wowote na kuanzishwa kwa Jumuiya ya Madola.

Hata hivyo, watahiniwa 289,693 (28.60%) waliweza kuchagua jibu sahihi E, 1931. Watahiniwa hao walikuwa na uelewa kuhusu majina, kipindi na sababu ya kuanzishwa kwa jumuiya mbalimbali za Kimataifa.

**Swali la 25:** Mkataba gani ulipunguza madaraka ya Sultan wa Zanzibar mwaka 1890?

A Mkataba wa Berlin
B Mkataba wa Frere
C Mkataba wa Heligoland
D Mkataba wa Moresby
E Mkataba wa Hamerton

Swali lilitoka katika mada ya *Uvamizi wa Afrika Kuanzia mwaka 1880.* Swali liliwataka watahiniwa kubaini jina la mkataba uliopunguza madaraka ya Sultan wa Zanzibar mwaka 1890. Kiwango cha ufaulu kwa watahiniwa katika swali hili kilikuwa cha wastani kwani watahiniwa 469,157 (46.30%) waliweza kuchagua jibu sahihi C, *Mkataba wa Heligoland*. Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mbinu na majina ya mikataba iliyotumiwa na Wajerumani na Waingereza kuigawa Afrika ya Mashariki kwa mara ya pili.

Pamoja na hayo, asilimia 37 ya watahiniwa waliokuwa na uelewa mdogo wa jinsi Afrika Mashariki ilivyogawanywa miongoni mwa mataifa ya Ulaya walichagua vipotoshi B, *Mkataba wa Frere*; D, *Mkataba wa Moresby* na E, *Mkataba wa Hamerton*. Watahiniwa hao walichagua majina ya mikataba iliyotumika katika kukomesha biashara ya utumwa katika Afrika Mashariki. Uchaguzi wa vipotoshi hivyo ni ushahidi kuwa baadhi ya watahiniwa walikuwa na uelewa mdogo kuhusu biashara ya utumwa na uvamizi wa Bara la Afrika. Kwa ujumla, watahiniwa hao walishindwa kutofautisha kati ya mikataba ya kukomesha biashara ya utumwa na mikataba iliyotumiwa na mataifa ya ulaya (Uingereza na Ujerumani) katika kuigawa Afrika Mashariki mara ya pili miongoni mwao.

Aidha, watahiniwa 159,807 (15.80%) walichagua kipotoshi A, *Mkataba wa Berlin*. Watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu dhana ya ukoloni na mbinu zilizotumiwa na Wajerumani na Waingereza kuigawa Afrika ya Mashariki. Huenda Mkataba wa Berlin ulichaguliwa kutokana na jukumu lililofanywa na mji wa Berlin katika kuandaa au kuwa mwenyeji wa mkutano kuanzia mwaka 1884 hadi 1885, chini ya uenyekiti wa Kansela Otto von Bismarck, ambao uliweka msingi wa kuligawa bara la Afrika miongoni mwa mataifa ya Ulaya.

Kwa ujumla, kutokana na uchaguzi wa vipotoshi hivyo, ni dhahiri kuwa watahiniwa hao hawakuelewa vizuri historia ya jinsi Afrika Mashariki ilivyogawanywa kwa mara ya pili kati ya Wajerumani na Waingereza. Kwa ufupi, watahiniwa hao walikosa maarifa juu ya kugawanywa kwa Afrika Mashariki.

**Swali la 26:** Ni nani alikuwa mwenyekiti wa kwanza wa Umoja wa Afrika?

A Thabo Mbeki
B Kwame Nkrumah
C Haile Selassie
D Mengistu Haile Mariam
E Salim Ahmed Salim

Swali hili liliwataka watahiniwa kubaini jina la kiongozi aliyekuwa mwenyekiti wa kwanza wa Umoja wa Afrika. Kiwango cha ufaulu kwa watahiniwa katika swali hili kilikuwa dhaifu kwani watahiniwa 869,257 (85.80%) hawakuweza kuchagua jibu sahihi.

Kipotoshi B, *Kwame Nkrumah* kilivutia zaidi ya robo ya watahiniwa (385,450, sawa na asilimia 38.00) waliojibu swali hili. Watahiniwa hao, walivutiwa na kipotoshi hiki kwa sababu walishindwa kutofautisha kati ya viongozi waliokuwa waanzilishi wa Umoja wa Nchi Huru za Kiafrika (OAU), ulioanzishwa mwaka 1963 mjini Addis Ababa (Ethiopia) na viongozi waliokuwa waanzilishi wa Umoja wa Afrika ulioanzishwa mwaka 2002 Durban (Afrika Kusini). Watahiniwa katika kundi hili walipaswa kuelewa kwamba Kwame Nkrumah hakushiriki kuanzisha Umoja wa Afrika mwaka 2002, bali alishiriki kuanzisha Umoja wa Nchi Huru za Kiafrika mwaka 1963. Kwame Nkrumah alifariki mwaka 1972 - miaka thelathini kabla ya kuundwa kwa Umoja wa Afrika. Hivyo, uchaguzi wa kipotoshi hiki unaashiria


kuwa watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mabadiliko ya kisiasa katika Afrika Huru na ushirikiano wa Kimataifa.

Kipotoshi kingine kilichovutia idadi kubwa ya watahiniwa ni C, *Haile Selassie*. Kipotoshi hiki kilivutia watahiniwa 165,846 (16.4%). Watahiniwa waliochagua kipotoshi hicho walishindwa kuelewa kuwa *Haile Selassie* hakuwa mwenyekiti wa kwanza wa Umoja wa Afrika (AU), bali alikuwa mwenyekiti wa kwanza wa Umoja wa Nchi huru za Kiafrika (OAU). Uchaguzi wa kipotoshi hiki unaashiria kuwa watahiniwa hao hawakuwa na uelewa wa majina ya viongozi waanzilishi, muda na tofauti kati ya OAU na AU.

Aidha, kipotoshi D, *Mengistu Haile Mariam,* kilivutia watahiniwa 253,148 (25.00%) ambao hawakuwa na uelewa wa jina la mwenyekiti wa kwanza wa Umoja wa Afrika. Watahiniwa hao, walipaswa kuelewa kuwa *Mengistu Haile Mariam* alimpindua Mfalme Haile Selassie kwa kumwaga damu mwaka 1974 na kuwa Rais wa Ethiopia. Watahiniwa huenda walivutiwa na kipotoshi hiki kwa sababu ya umaarufu wa *Mengistu Haile Mariam* – Mwanajeshi na Rais dikteta wa Ethiopia (1974 – 1991) aliyefahamika kwa ukatili wake.

Kipotoshi E, *Salim Ahmed Salim* kilichaguliwa na watahiniwa ambao hawakuelewa kuwa Salim Ahmed Salim alikuwa Katibu Mkuu wa Umoja wa Nchi Huru za Kiafrika kuanzia mwaka 1989 hadi 2001-mwaka mmoja kabla ya Umoja wa Nchi Huru za Kiafrika (OAU) kubadilishwa na kuwa Umoja wa Afrika (AU) mwaka 2002. Watahiniwa hao walitakiwa kukumbuka kwamba Salim Ahmed Salim hakuwa mwenyekiti wa Umoja wa Nchi Huru za Kiafrika (OAU) au Umoja wa Afrika (AU).

Pamoja na hayo, ni watahiniwa 143,807 (14.20%) tu waliweza kuchagua jibu sahihi A, *Thabo Mbeki*. Watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu miaka ambayo Umoja wa Nchi Huru za Kiafrika (OAU) na Umoja wa Afrika (AU) zilianzishwa pamoja na majina ya viongozi waanzilishi. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kimeoneshwa katika Chati Na. 12.





**Chati Na. 12:** *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 26.*

### 2.1.3. Kipengele III: Jiografia

**Swali la 27:** Lipi kati ya yafuatayo linatokana na dunia kujizungusha katika mhimili wake?

A Kupatwa kwa jua
B Kupatwa kwa mwezi
C Usiku na mchana
D Majira ya mwaka
E Tofauti ya muda kati ya usiku na mchana

Swali hili lilitoka katika mada ya *Mfumo wa Jua.* Swali liliwataka watahiniwa kubainisha matokeo ya Dunia kujizungusha katika mhimili wake. Kiwango cha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili kilikuwa kizuri kwani jumla ya watahiniwa 722,917 (71.36%) walichagua jibu sahihi *C, Usiku na mchana*. Watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu matokeo ya kitendo cha dunia kujizungusha katika katika mhimili wake. Chati Na. 13 inaonesha asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.




**Chati Na. 13:** *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 27*

Watahiniwa 49,062 (4.84%) walichagua kipotoshi *A, Kupatwa kwa jua.* Watahiniwa hao walishindwa kutambua namna kupatwa kwa jua kunavyotokea. Kupatwa kwa jua hutokea pale ambapo mwezi unakuwa katikati ya dunia na jua, jambo ambalo husababisha mwanga wa jua usifike baadhi ya sehemu ya Dunia. Watahiniwa hao walitakiwa kufahamu kuwa kupatwa kwa jua husababishwa na kitendo cha Dunia kulizunguka Jua na si kujizungusha katika mhimili wake.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 46,121 (4.55%) walichagua kipotoshi *B, kupatwa kwa mwezi*, tukio ambalo ni matokeo ya dunia kulizunguka jua. Tukio hili hutokea wakati dunia ipo katikati ya mwezi na jua, hivyo kuzuia mwanga wa jua usiufikie mwezi. Pia, watahiniwa 148,767 (14.68%) waliochagua kipotoshi *D, majira ya mwaka*. Watahiniwa hao walishindwa kutambua kuwa ili kupata majira ya mwaka kunahitajika siku 365¼/366; muda huu hutumiwa na dunia kulizunguka jua. Uchaguzi wa kipotoshi hiki unaonesha kuwa watahiniwa hawa walikosa maarifa ya kutosha juu ya matokeo ya dunia kujizungusha kwenye mhimili wake na kulizunguka jua.

Aidha, watahiniwa 39,466 (3.90%) walichagua kipotoshi *E, tofauti ya muda kati ya usiku na mchana*. Watahiniwa hawa walishindwa kutofautisha uwepo wa nuru na giza na utofauti wa urefu wa usiku au mchana. Utofauti wa muda wa mchana na usiku husababishwa na kitendo cha dunia kulizunguka jua. Jua likiwa la utosi katika kizio cha kaskazini husababisha mchana kuwa mrefu na usiku kuwa mfupi wakati huo, ilhali katika kizio cha kusini mchana huwa mfupi na usiku huwa mrefu.

**Swali la 28:** Lipi kati ya yafuatayo ni matokeo ya ukame wa muda mrefu?

A Mafuriko  B Kimbunga
C Tetemeko la ardhi  D Njaa
E Magonjwa

**Jedwali Na. 12: Idadi na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo**

| Chaguo | A | B | C | D* | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya Watahiniwa** | 72,961 | 104,673 | 115,026 | 661,029 | 51,768 | 7,607 |
| **Asilimia ya Watahiniwa** | 7.20 | 10.33 | 11.35 | 65.25 | 5.11 | 0.75 |

Katika Jedwali Na. 12, kiwango cha ufaulu ni kizuri kwani 65.25% ya watahiniwa walichagua jibu sahihi.


Swali hili lilitoka katika mada ya *Majanga*. Swali lilipima uwezo wa watahiniwa kutambua jambo linalosababishwa na ukame wa muda mrefu. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa kwa kiwango kizuri, kwani jumla ya watahiniwa 661,029 (65.25%) waliweza kuchagua jibu sahihi *D, Njaa*. Watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu majanga mbalimbali na madhara yake.

Watahiniwa walioshindwa kuchagua jibu sahihi hawakuwa na uelewa wa kutosha katika mada ya *majanga.* Hivyo, walishindwa kuhusianisha ukame na njaa. Watahiniwa hao walitakiwa kutambua kuwa ukame wa muda mrefu husababisha kukauka kwa mimea na vyanzo vya maji hivyo hupelekea kutokea kwa njaa. Watahiniwa wengine 72,961 (7.20%) walichagua kipotoshi *A, Mafuriko;* walishindwa kubaini kuwa mafuriko ni matokeo ya mvua kubwa. Watahiniwa 104,673 (10.33%) walichagua kipotoshi *B, Kimbunga.* Watahiniwa hao walishindwa kubaini kuwa kimbunga ni upepo mkali na wenye kasi. Watahiniwa 115,026 (11.35%) walichagua kipotoshi *C, Tetemeko la ardhi.* Huu ni mtikisiko wa ardhi unaosababishwa na nguvu ya uvutano ardhini. Pia, watahiniwa 51,768 (5.11%) waliochagua *E, Magonjwa,* walishindwa kubaini kuwa magonjwa ni matokeo ya uchafuzi wa mazingira na si matokeo ya ukame wa mda mrefu.

**Swali la 29**: Yapi ni madhara ya Utalii?

A Kusambaa kwa magonjwa
B Kupungua kwa misitu
C Kupungua kwa mvua
D Kupungua kwa rutuba ya udongo
E Kupungua kwa wanyama pori

Swali hili lilitoka katika mada ya *shughuli za kiuchumi*. Swali lilipima uwezo wa watahiniwa katika kutambua madhara yatokanayo na shughuli za utalii. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa wa kiwango kizuri; jumla ya watahiniwa 655,111 (64.67%) waliweza kuchagua jibu sahihi *A, Kusambaa kwa magonjwa.* Kusambaa kwa magonjwa huweza kutokea ambapo watu wanaokwenda kutalii au wenyeji wa eneo husika wana vimelea vya magonjwa. Vimelea hivi huweza kubebwa kutoka eneo moja hadi jingine kwa kuwa mtalii husafiri kutoka eneo moja kwenda jingine. Chati Na. 14 inaonesha asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.




**Chati 14***: Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 29*

Watahiniwa 60,114 (5.93%) walichagua kipotoshi *B, Kupungua kwa misitu.* Watahiniwa hao walishindwa kubaini kuwa kupungua kwa misitu hakusababishwi na utalii kwani utalii husababisha utunzaji wa misitu. Kupungua kwa misitu kunatokana na kilimo, ujenzi wa miundombinu, ujenzi wa makazi ya watu, majanga ya asili kama vile moto na mlipuko wa volcano. Pia, watahiniwa waliochagua kipotoshi *C, Kupungua kwa mvua (*3.39%) walishindwa kubaini kuwa mvua hupungua kutokana na mabadiliko ya tabianchi ambayo husababishwa na shughuli mbalimbali za binadamu kama vile

uzalishaji viwandani, uchomaji mkaa, kilimo cha kutumia kemikali na matumizi ya silaha mbalimbali za kivita.


Pia, watahiniwa 52,763 (5.21%) waliochagua kipotoshi *D, kupungua kwa rutuba ya udongo.* Watahiniwa hao walishindwa kutambua kuwa rutuba hupungua kutokana na matumizi ya mbolea za viwandani, kulima eneo moja au zao moja kwa muda mrefu na kuchimba madini. Aidha, watahiniwa 202,663 (20.00%) walichagua *E, Kupungua kwa wanyamapori.* Watahiniwa hao walishindwa kubaini kuwa wanyamapori hupungua kutokana na mabadiliko ya tabianchi, uwindaji haramu na majanga ya asili.

**Swali la 30:** Vipi ni viumbe hai vinavyoishi majini?

| | | | |
|---|---|---|---|
| A | Samaki na kiboko | B | Kiboko na twiga |
| C | Kipepeo na samaki | D | Swala na kiboko |
| E | Twiga na chura | | |

Swali hili lilitoka katika mada ya *Mazingira.* Swali lilipima uwezo wa watahiniwa kubaini majina ya viumbe wanaoishi kwenye maji. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa mzuri kwani jumla ya watahiniwa 938,397 (92.63%) waliweza kuchagua jibu sahihi *A, Samaki na Kiboko*. Watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu mazingira wanayoishi viumbe mbalimbali.

Uchambuzi zaidi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa jumla ya watahiniwa 19,773 (1.95%) walichagua vipotoshi *B, Kiboko na twiga*; 21,277 (2.10%), *C, Kipepeo na samaki*; 21,277 (2.10%), *D, Swala na kiboko*; *na* 13,950 (1.38%), *E, Twiga na chura*. Uchaguzi wa vipotoshi hivi unaonesha kuwa watahiniwa hao hawakuwa na ufahamu wa kutosha kuhusu makazi ya viumbe mbalimbali. Watahiniwa hao walishindwa kutambua kuwa vipepeo huishi kwenye miti na mapangoni, wakati swala na twiga huishi nchi kavu sehemu zenye vichaka vidogo. Watahiniwa 5,744 (0.56%) hawakujibu swali hili au walichagua jibu zaidi ya moja. Chati Na.15 inaonesha asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo.





**Chati Na. 15***: Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 30*

**Swali la 31:** Mistari ya gridi katika ramani husomwa kuanzia

A mistari ya ulalo halafu wima.
B mistari ya latitudo halafu longitudo.
C mistari ya wima halafu ulalo.
D mistari ya ulalo halafu longitudo.
E mistari ya wima halafu latitudo.

Swali hili lilitungwa kutoka katika mada ya *Stadi za Ramani.* Swali lilipima uwezo wa watahiniwa katika kubaini namna sahihi ya usomaji wa mistari ya gridi. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ni wa wastani kwani watahiniwa 491,107 (48.48%) walichagua jibu sahihi *C, mistari ya wima halafu ulalo.* Watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu usomaji wa mistari ya gridi. Mistari ya gridi husomwa kwa kuanza na mistari ya wima ambayo namba zake huongezeka kuelekea mashariki. Kisha hufuatiwa na mistari ya ulalo ambayo namba zake huongezeka kuelekea kaskazini. Chati Na. 16 inaonesha asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo.





**Chati Na. 16:** *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 31*

Jumla ya watahiniwa 347,603 (34.31%) walichagua kipotoshi *A, Mistari ya ulalo halafu wima.* Hili halikuwa chaguo sahihi kwa sababu mistari inayochorwa kwa ulalo namba zake huandikwa na kusomwa kwa wima na ya wima namba zake huandikwa kwa ulalo. Hivyo, watahiniwa wengi walichanganya namna ya usomaji wake; *B Mistari ya latitudo halafu longitudo* (107,205 sawa na 10.58%); *D, Mistari ya ulalo halafu longitudo* (27,234 sawa na 2.69%) na *E, Mistari ya wima halafu latitudo* (30,539 sawa na 3.01%). Watahiniwa hao hawakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu usomaji wa mistari ya gridi. Watahiniwa 9,376 (0.93%) waliobaki hawakujibu swali hili au walichagua jibu zaidi ya moja.

**Swali la 32:** Ni kitu gani hutumika kufafanua alama zilizotumika katika ramani?

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| A | Dira | B | Kipimio | C | Jina la ramani |
| D | Fremu | E | Ufunguo | | |

Swali lilitoka katika mada ya *Stadi za ramani*. Watahiniwa walitakiwa kubainisha kitu kinachomwezesha msoma ramani kutambua alama zilizotumika katika ramani husika. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa mzuri kwani watahiniwa 709,552 (70.04%) waliweza kuchagua jibu sahihi *E, Ufunguo.* Watahiniwa hao walikuwa na ujuzi wa kutosha katika kusoma na kutafsiri ramani. Chati Na. 17 inaonesha asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.




**Chati Na. 17:** *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 32*

Uchambuzi zaidi wa swali hili unaonesha kuwa watahiniwa 117,499 (11.60%) walichagua kipotoshi *A, Dira*. Wanafunzi hao walishindwa kuelewa kuwa dira inatumika kutambua uelekeo wa kaskazini katika ramani tu na haina uwezo wa kumfanya msomaji kutambua kila kitu kilichopo katika ramani. Jumla ya watahiniwa 89,739 (8.86%) walichagua kipotoshi *B, Kipimio*. Kipimio kinamsaidia msomaji wa ramani kutambua uhusiano uliopo kati ya umbali katika ramani na umbali halisi katika ardhi. Kwa upande mwingine, watahiniwa 41,364 (4.08%) walichagua kipotoshi *C, Jina la ramani,* ambalo humwezesha msomaji kufahamu ramani husika inahusu nini lakini haimpi fursa ya kutambua maana ya alama zilizomo kwenye ramani husika. Aidha, jumla ya *w*atahiniwa 45,428 (4.48%) walichagua kipotoshi *D, Fremu*. Watahiniwa hao walishindwa kuelewa kuwa swali liliwataka kubaini kitu kitakachowawezesha wasoma ramani kutambua maana ya alama na si mipaka ya ramani husika. Watahiniwa 9,515 (0.93%) hawakujibu swali hili au walichagua jibu zaidi ya moja.

**Swali la 33:** Dira ikitulia mshale wake huonesha upande gani?

A Mashariki B Magharibi C Kaskazini
D Kusini E Kusini Magharibi

**Jedwali Na.13: Idadi na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo**

| Chaguo | A | B | C* | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya Watahiniwa** | 131,238 | 111,544 | 588,902 | 101,296 | 69,186 | 10,898 |
| **Asilimia ya Watahiniwa** | 12.95 | 11.01 | 58.13 | 10.00 | 6.83 | 1.08 |

Katika Jedwali Na. 13, kiwango cha ufaulu ni cha wastani kwani asilimia 58.13 ya watahiniwa walichagua jibu sahihi.

Swali hili lilitungwa kutoka katika mada inayohusu *Stadi za ramani*. Watahiniwa walitakiwa kubainisha upande ambao mshale wa dira huonesha ikiwa umetulia. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa wa kiwango cha wastani kwani watahiniwa 588,902 (58.13%) walichagua jibu sahihi *C, Kaskazini*. Watahiniwa hao walikuwa na ufahamu wa kutosha kuhusu usomaji wa dira. Dira inapokuwa imetulia, huonesha upande wa kaskazini. Hii inatokana na nguvu ya uvutano iliyopo baina ya sumaku iliyopo kwenye dira na ile iliyopo kwenye ncha ya kaskazini ya dunia.


Kwa upande mwingine, watahiniwa 413,264 (41.87%) walikosa swali hili kwa kuchagua vipotoshi vifuatavyo: *A, Mashariki (12.95%); B, Magharibi (11.01%)*; *D, Kusini (10.00*%) *na E, Kusini Magharibi (6.83*%)*.* Watahiniwa hao walishindwa kubaini kuwa vipotoshi hivi vinahusiana na pande kuu za dunia ambazo huwa hazioneshwi kwa uwazi na mshale wa dira ikiwa imetulia. Jumla ya watahiniwa 10,898 (1.08%) hawakujibu swali hili au walichagua jibu zaidi ya moja.

**Swali la 34:** Namba ipi hupewa mstari wa kontua unaochorwa kuwakilisha usawa wa bahari?

A 20 B 5 C 15
D 0 E 4

Swali lilitoka katika mada ya *Stadi za ramani* na lilipima uwezo wa watahiniwa kubaini namba na mstari wa kontua unaochorwa kuwakilisha usawa wa bahari. Kiwango cha ufaulu cha watahiniwa katika swali hili kilikuwa kizuri kwani watahiniwa 694,509 (68.6%) walichagua jibu sahihi *D, 0.* Watahiniwa hao walikuwa na ufahamu

wa kutosha kuhusu uchoraji na usomaji wa mistari ya kontua. Mstari ambao huchorwa kuwakilisha usawa wa bahari hupewa namba 0. Chati Na. 18. inaonesha asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.




**Chati Na. 18**: *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 34.*

Kwa upande mwingine, watahiniwa 305,822 (30.1%) walichagua vipotoshi *A, 20 (*5.0%); *B, 5 (*8.7%)*; C, (12.4%)* na *E, 4 (4.2%).* Uchaguzi wa vipotoshi hivi unaonesha ufinyu wa maarifa waliyokuwa nayo watahiniwa kuhusiana na uchoraji na usomaji wa mistari ya kontua.

**Swali la 35:** Chanzo cha maji kinachoweza kutumika kuzalisha chumvi ni

A mvua. B mto. C chemchemi.
D bahari. E bwawa.

**Jedwali Na. 14: Idadi na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo**

| Chaguo | A | B | C | D* | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya Watahiniwa** | 78,125 | 78,851 | 221,031 | 558,621 | 66,494 | 9,942 |
| **Asilimia ya Watahiniwa** | 7.71 | 7.78 | 21.82 | 55.14 | 6.56 | 0.98 |

Katika Jedwali Na. 14, kiwango cha ufaulu ni cha wastani kwani asilimia 55.14 ya watahiniwa walichagua jibu sahihi.


Swali hili lilitoka katika mada ya *Maji* na liliwataka watahiniwa kubainisha jina la chanzo cha maji ambacho hutumika kuzalisha chumvi. Kiwango cha ufaulu cha watahiniwa katika swali hili ni cha wastani kwani watahiniwa 558,621 (55.14%) walichagua jibu sahihi *D, Bahari.* Watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa kutosha juu ya vyanzo vya maji vinavyoweza kutumika kuzalisha chumvi. Maji ya bahari kwa asili ni maji magumu ambayo yana chumvi; hivyo, hutumika katika uzalishaji wa chumvi.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 444,501 (43.86%) hawakuelewa matakwa ya swali. Kwa mfano, watahiniwa 78,125 (7.71%) walichagua *A, Mvua*; 78,851 (7.78%) walichagua *B, Mto*; 221,031 (21.82%) walichagua *C, Chemchem* na watahiniwa 66,494 (6.56%) walichagua *E, Bwawa*. Watahiniwa hao walishindwa kubaini kuwa mvua huzalisha maji laini na safi. Mto ambao ni maji yatiririkayo kutoka milimani kuelekea baharini au ziwani pia chanzo chake ni mvua au chemchem ambayo pia ni maji laini. Aidha, bwawa ni sehemu ya ardhi iliyochimbwa kwa lengo la kuhifadhi maji kwa ajili ya matumizi mbalimbali. Chanzo chake kinaweza kuwa mvua, mto au ziwa. Maji kutoka katika vyanzo hivi hayazalishi chumvi kwani ni maji laini. Watahiniwa 9,942 (0.98%) hawakujibu swali hili au walichagua majibu zaidi ya moja.

**Swali la 36:** Ni shughuli gani huchangia kupungua kwa misitu?

A Kilimo cha kubadilisha mazao
B Ukataji wa miti kwa ajili ya mkaa
C Kupanda miti sehemu iliyokatwa
D Kupanda miti sehemu iliyokosekana
E Elimu ya mazingira

Swali hili lilitoka katika mada ya *Mazingira*. Swali liliwataka watahiniwa kubainisha shughuli inayochangia kupungua kwa misitu. Kiwango cha ufaulu cha watahiniwa kilikuwa kizuri kwani watahiniwa 879,536 (86.82%) walichagua jibu sahihi *B*, *Ukataji wa miti kwa ajili ya mkaa.* Watahiniwa hao walielewa kuwa ili kuweza kuandaa mkaa, ni lazima ukate miti na kuipanga kwenye tanuri kisha kuwasha moto ndipo upate mkaa. Kitendo hiki husababisha kupungua kwa misitu kwani miti mikubwa na midogo hukatwa. Chati Na. 19 Inaonesha asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.




**Chati Na. 19**: *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 36*


Jumla ya watahiniwa 38,425 (3.79%) walichagua kipotoshi *A, Kilimo cha kubadilisha mazao*. Watahiniwa hao walishindwa kutambua kuwa kilimo cha kubadilisha mazao ni njia bora ya kuhifadhi rutuba katika shamba. Watahiniwa 33,164 (3.27%) walichagua kipotoshi *C, Kupanda miti sehemu iliyokatwa*. Watahiniwa hawa walishindwa kuelewa matakwa ya swali. Swali liliwataka kutoa sababu ya kupungua kwa misitu kutoka katika machaguzi waliyopewa lakini watahiniwa hao walitoa njia za kutunza mazingira.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 32,824 (3.24%) walichagua kipotoshi *D, Kupanda miti sehemu iliyokosekana*. Watahiniwa hawa hawakuelewa lengo kuu la swali kwani kitendo cha kupanda miti huongeza ukubwa wa eneo la msitu. Aidha, jumla ya watahiniwa 21,336 (2.11%) walichagua kipotoshi *E, Elimu ya mazingira*. Watahiniwa hawa walishindwa kuelewa kuwa elimu huwasaidia watu kutambua njia bora za utunzaji wa misitu. Watahiniwa wengine 7,779 (0.77%) hawakujibu swali hili au walichagua jibu zaidi ya moja.

**Swali la 37:** Kitendo cha kupeleka ujumbe kutoka kwa mtu mmoja kwenda kwa mwingine huitwa

| | | |
|---|---|---|
| A uchukuzi. | B utalii. | C mawasiliano. |
| D utandawazi. | E uhamaji. | |

Swali hili lilitoka katika mada ya *Mawasiliano, biashara na uchukuzi.* Katika kujibu swali hili, watahiniwa walitakiwa kubaini njia inayotumika kupeleka ujumbe kutoka kwa mtu mmoja kwenda kwa mwingine. Kiwango cha ufaulu cha watahiniwa katika swali hili kilikuwa kizuri kwani watahiniwa 833,802 (82.30%) walichagua jibu sahihi *C*, *mawasiliano.* Watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu mada ya mawasiliano. Chati Na. 20 inaonesha wastani wa watahiniwa katika kila chaguo.




**Chati Na. 20**: *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 37*

Watahiniwa wengine 170,702 (16.75%) hawakuelewa matakwa ya swali. Watahiniwa hao walivutiwa na vipotoshi *A, uchukuzi* (6.30%); *B, utalii* (3.57%); *D, utandawazi* (4.98%); na *E, uhamiaji* (2.00%). Watahiniwa hao walipaswa kuelewa kuwa, kwa upande mmoja, uchukuzi ni kitendo cha kusafirisha watu au bidhaa kutoka sehemu moja kwenda nyingine. Kwa upande mwingine utalii ni kitendo cha kusafiri kutoka eneo moja kwenda jingine kwa lengo la kujifunza, kuburudika au kupumzika; utandawazi ni mfumo unaounganisha watu katika nyanja za kiuchumi, kisiasa na kijamii; bali Uhamiaji ni kitendo cha kutoka eneo moja kwenda kuishi eneo lingine. Vipotoshi vyote vinahusisha kusafiri kutoka eneo moja hadi lingine lakini havihusiani na kupeleka ujumbe kutoka kwa mtu mmoja kwenda kwa mwingine. Watahiniwa wengine 8,560 (0.84%) hawakujibu swali hili au walichagua jibu zaidi ya moja.

**Swali la 38:** Shughuli za biashara zina faida gani?

A Kuongeza pato la Taifa
B Ongezeko la mvua
C Kupungua kwa migogoro
D Kupungua kwa wakimbizi
E Ongezeko la wanyamapori

**Jedwali Na.15: Idadi na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo**

| Chaguo | A* | B | C | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya Watahiniwa** | 890,550 | 33,264 | 44,260 | 21,267 | 17,051 | 6,672 |
| **Asilimia ya Watahiniwa** | 87.91 | 3.28 | 4.37 | 2.10 | 1.68 | 0.66 |

Katika Jedwali Na. 15, kiwango cha ufaulu ni kizuri kwani asilimia 87.91 ya watahiniwa walichagua jibu sahihi.

Swali hili lilitoka katika mada ya *Mawasiliano, biashara na uchukuzi*. Watahiniwa walitakiwa kubainisha faida zitokanazo na shughuli za biashara. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa wa kiwango kizuri kwani watahiniwa 890,550 (87.91%) walichagua jibu sahihi *A, Kuongeza pato la taifa*. Watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu faida ya shughuli za kibiashara. Hivyo, walitambua kuwa kitendo cha kuuza na kununua bidha au huduma huzalisha faida ambayo huliongezea taifa kipato kwa njia ya kodi.


Aidha, chaguo *B, Ongezeko la mvua* lilichaguliwa na watahiniwa 33,264 (3.28%). Watahiniwa hao walishindwa kubaini kuwa ongezeko la mvua hutokana na kuongezeka kwa mvukizo wa maji kutoka kwenye mimea, ardhi na vyanzo vya maji. Hivyo, hakuhusiani na kuongezeka kwa biashara. Pia, watahiniwa 44,260 (4.37%) walichagua kipotoshi *C, kupungua kwa migogoro.* Kipotoshi hiki kilichaguliwa kwa kiasi kikubwa kulingana na ukweli kuwa uwepo wa utulivu na amani huwezesha kufanyika kwa shughuli mbalimbali za kiuchumi isipokuwa si lazima kuwa migogoro kuathiri moja kwa moja uendeshaji wa biashara. Pia watahiniwa 21,267 (2.10%) waliochagua *D, kupungua kwa wakimbizi.* Kipotoshi hiki si sahihi kwani kupungua kwa wakimbizi husababishwa na kupatikana kwa amani kwenye eneo wanalotoka. Aidha, jumla ya watahiniwa 17,051 (1.68%) walichagua *E, ongezeko la wanyamapori*. Watahiniwa hao

walishindwa kubaini kuwa kuongezeka kwa wanyamapori kunatokana na utunzaji wa maliasili. Pia, kuongezeka kwa wanyamapori huvutia utalii hivyo watahiniwa hawa walidhani kuwa ni faida ya biashara.

**Swali la 39:** Vifaa vipi vya usafirishaji vinatumika majini?

A Treni, meli na boti
B Meli, boti na mtumbwi
C Pikipiki, basi na meli
D Ndege, treni na basi
E Meli, boti na ndege

Swali hili lilitoka katika mada ya *Mawasiliano, biashara na uchukuzi.* Watahiniwa walitakiwa kubainisha vifaa vya usafirishaji vinavyotumika majini. Kiwango cha ufaulu cha watahiniwa katika swali hili kilikuwa kizuri kwani watahiniwa 886,534 (87.51%) waliweza kuchagua jibu sahihi *B, Meli, boti na mtumbwi*. Watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa vifaa vinavyotumika kwa usafirishaji katika maji. Chati Na. 21 inaonesha asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.




**Chati Na. 21:** *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 39*


Kwa upande mwingine, watahiniwa walichagua kipotoshi *A, Treni, meli na boti* (5.06%); *C, Pikipiki, basi na meli* (2.80%); *D, Ndege, treni na basi* (2.42%) na *E, Meli, boti na ndege* (1.57%). Watahiniwa hao walishindwa kubaini kuwa treni, pikipiki na basi hutumika kwa usafirishaji katika nchi kavu na ndege hutumika kwa usafirishaji angani. Watahiniwa hawa kwa ujumla hawakuwa na maarifa ya

kutosha kutambua njia mbalimbali za usafirishaji na vyombo vinavyotumika. Watahiniwa wengine 6,429 (0.63%) hawakujibu swali hili au walichagua jibu zaidi ya moja.

**Swali la 40:** Zifuatazo ni faida za matumizi mrudio ya taka, isipokuwa

A watu kupata ajira.
B utunzaji wa maliasili.
C hupunguza ongezeko la joto duniani.
D ongezeko la rutuba katika udongo.
E kupunguza kuenea kwa magonjwa.

Swali hili lilitoka katika mada ya *Mazingira.* Watahiniwa walitakiwa kubainisha jambo ambalo si faida ya matumizi mrudio ya taka kutoka kwenye machaguo waliyopewa. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa hafifu kwani ni watahiniwa 209,296 (20.66%) tu waliweza kuchagua jibu sahihi *D, ongezeko la rutuba katika udongo*. Watahiniwa waliochagua jibu sahihi walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu faida za matumizi ya taka mrejeo. Watahiniwa hawa walitambua kuwa kuongezeka kwa rutuba katika udongo siyo faida ya moja kwa moja ya matumizi ya taka mrejeo. Chati Na. 22 inaonesha asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.




**Chati Na. 22:** *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 40*


Watahiniwa 221,222 (21.84%) walichagua kipotoshi *A, watu kupata ajira*. Watahiniwa hao walishindwa kubaini kuwa watu kupata ajira ni faida mojawapo ya matumizi mrudio ya taka. Watu hufanya kazi ya

kukusanya taka kama vile chupa za maji zilizotumika na vipande vya bati au chuma ambavyo huviuza na kujipatia fedha. Jumla ya watahiniwa 138,644 (13.69%) walichagua kipotoshi *B, utunzaji wa maliasili.* Watahiniwa hao walishindwa kubaini kuwa taka huathiri makazi ya viumbe hai na kuvifanya vipotee kabisa. Hivyo, taka mrudio hufanya makazi hayo kuwa salama na rafiki kwa viumbe hai. Kipotoshi *C, hupunguza ongezeko la joto duniani*, kilivutia watahiniwa 281,057 (27.74%), ambao walishindwa kubaini kuwa matumizi ya taka mrejeo hupunguza uzalishaji wa taka hasa zile za plastiki ambazo huzuia mionzi ya jua kusharabiwa katika ardhi hivyo kurudishwa angani na kusababisha kuharibiwa kwa tabaka la ozoni. Tabaka la ozoni ndilo hufanya kazi ya kupunguza makali ya mionzi ya jua. Linapoharibiwa, joto huongezeka duniani. Pia, watahiniwa 151, 515 (14.96%) walichagua kipotoshi *E, Kupunguza kuenea kwa magonjwa.* Watahiniwa hao walishindwa kubaini kuwa taka mrejeo hupunguza kuenea kwa magonjwa kwani magonjwa mengi yana uhusiano wa moja kwa moja na mazingira machafu. Vipotoshi hivyo vilikuwa ni faida za matumizi ya taka mrejeo.

## 2.2 Sehemu B


**Swali la 41:** Kwa nini serikali inapiga vita matumizi ya baruti katika shughuli za uvuvi?

Swali lilitoka katika mada ya *Uchumi Wetu* na liliwataka watahiniwa kutoa sababu za serikali kupiga vita matumizi ya baruti katika shughuli za uvuvi. Ufaulu katika swali hili ulikuwa mzuri; watahiniwa 635,075 (62.97%) walipata alama zote 2 za swali hili; watahiniwa 86,361 (8.56%) walipata alama 1; na watahiniwa wengine 287,036 (28.46%) walipata alama 0. Chati Na. 23 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali la 41.




**Chati Na.23:** *Ufaulu mzuri wa watahiniwa katika swali la 41*

Watahiniwa waliopata alama zote 2 (62.97%) walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu sababu za serikali kupiga vita matumizi ya baruti katika shughuli za uvuvi. Watahiniwa hao walielewa kuwa katazo hilo la serikali linalenga kunusuru maisha ya viumbe hai katika maji na mazingira yao ambayo hutumiwa na samaki kuzaliana. Hii ni kwa sababu baruti huua samaki wakubwa na wadogo ambao hawahitajiki kuvuliwa, baruti husababisha uchafuzi wa mazingira na huharibu vyanzo vya maji. Kielelezo Na. 1 sampuli kutoka katika majibu ya mtahiniwa aliyeweza kubaini matakwa ya swali la 41.



41. Kwa nini serikali inapiga vita matumizi ya baruti katika shughuli za uvuvi?
Kwa sababu huhatalisha viumbe hai vya majini na uhalibifu wa mazingira

**Kielelezo Na.1:** *Sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kubaini matakwa ya swali*

Hata hivyo, asilimia 8.56 ya watahiniwa waliopata alama 1 walishindwa kutoa maelezo yenye uzito wa kutosha kuweza kupata alama zote 2 za swali hili. Baadhi ya maelezo waliyotoa ni serikali inapiga vita matumizi ya baruti katika shughuli za uvuvi kwa kuwa ni haramu bila kutoa maelezo ya kina sababu zilizopelekea kuwa ni haramu.

Kwa upande mwingine, asilimia 28.46 ya watahiniwa walishindwa kubaini matakwa ya swali, hivyo kupata alama 0. Baadhi ya hoja ambazo zilitolewa zilihusisha hoja ya vita dhidi ya matumizi ya baruti

na vita vya kupigania uhuru. Mtahiniwa mmoja alisema *ili nchi zipate uhuru wake zingine zilipigana kwa njia ya bunduki au kwa njia ya katiba.* Mwingine alisema *kwa sababu watu wapate uhuru.* Mwingine, alihusisha baruti na aina za nyavu na kudai *ni nyavu ambazo siyo salama kuvulia samaki.* Vilevile, mwingine alidai *baruti ni uvuvi wa kutumia nyavu ndogo unaovua samaki wadogo tu.* Aidha, kuna mtahiniwa mmoja alihusisha baruti na Alama za Taifa kwa kutoa hoja *baruti ni kitambulisho cha serikali katika ngao za pili ya Zanzibar.* Majibu yote hayo hayakuwa sahihi, na hii inaonesha kuwa watahiniwa hao walikosa maarifa ya kutosha. Mwisho, kuna baadhi ya watahiniwa walikosa stadi za kusoma na kuandika ambapo waliandika vitu visivyoeleweka au kutojibu kabisa swali hili. Kielelezo Na. 2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kubaini matakwa ya swali la 41.



41. Kwa nini serikali inapiga vita matumizi ya baruti katika shughuli za uvuvi?

Kwa Sababu baruti ni Kitambulisho cha Serikali Katika ngao ya pili ya Zanzibar.

**Kielelezo Na.2:** *Sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kubaini matakwa ya swali*

**Swali la 42:** Mwanadamu wa mwanzo alitengenezaje moto?


Swali liliwataka watahiniwa kueleza njia ambazo mwanadamu wa mwanzo alitumia kutengeneza moto. Kiwango cha ufaulu kwa watahiniwa katika swali hili kilikuwa kizuri kwani watahiniwa 651,986 (64.65%) waliweza kueleza jinsi mwanadamu wa mwanzo alivyoweza kutengeneza moto. Watahiniwa katika kundi hili walieleza kuwa moto ulitengenezwa ama kwa kugonganisha mawe au kwa kufikicha kijiti kwenye mti uliokauka. Kwa ujumla, watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa ugunduzi uliofanywa na mwanadamu pamoja na manufaa ya ugunduzi huo katika kipindi cha zama za kati za mawe.




**Chati Na. 24:** *Inaonesha ufaulu wa kiwango kizuri (64.65%) kwa watahiniwa waliofanya swali hili.*

Vilevile, jumla ya watahiniwa 69,867 (6.9%) walipata alama moja katika swali hili. Watahiniwa walio wengi katika kategoria hii waliweza kueleza jinsi moto ulivyotengenezwa kwa kupekecha kijiti chembamba kikavu kiitwacho ulindi katika gogo kubwa lililokauka liitwalo uwimbombo. Watahiniwa wachache waliweza kueleza jinsi moto ulivyopatikana kwa kugonganisha mawe. Kwa ujumla watahiniwa katika kategoria hii waliandika jibu moja lililokuwa sahihi.

Aidha, jumla ya watahiniwa 286,619 (28.4%) walipata sifuri kwa sababu walikuwa na uelewa mdogo kwenye mada iliyotahiniwa. Baadhi ya watahiniwa katika kategoria hii, waliorodhesha zama tatu za mawe; wengine walieleza faida zilizotokana na ugunduzi wa moto. Baadhi ya majibu yasiyo sahihi yaliyotolewa na watahiniwa ni kama ilivyooneshwa kwenye Kielelezo Na.3.


42. Mwanadamu wa mwanzo alitengenezaje moto?

Ali tenge ne Moto Katika
Zama Kati Zamawe

***Kielelezo Na* 3:** *Sampuli ya majibu yasiyo sahihi*.

**Swali la 43:** Kwa nini Tanganyika iliondolewa katika utawala wa Ujerumani na kuwekwa chini ya utawala wa Kiingereza karne ya 20?

Swali hili liliwataka watahiniwa kueleza sababu iliyofanya Tanganyika kuondolewa katika utawala wa Ujerumani na kuwekwa chini ya utawala wa Kiingereza katika karne ya 20. Kiwango cha ufaulu kwa watahiniwa katika swali hili kilikuwa ni dhaifu kwani watahiniwa wengi (868,076, sawa na asilimia 86.1) walipata alama sifuri. Watahiniwa katika kategoria hii walionesha ukosefu wa maarifa kwenye mada iliyotahiniwa. Baadhi ya majibu yasiyo sahihi yaliyotolewa na watahiniwa ni pamoja na sababu za kuanzishwa kwa utawala wa mlango wa nyuma katika Tanganyika, majukumu ya vitangulizi vya ukoloni katika kueneza ukoloni katika Tanganyika, sababu za kukomeshwa kwa biashara ya utumwa na sababu zilizopelekea muungano wa Tanganyika na Zanzibar. Majibu haya yasiyo sahihi yanaonesha kuwa watahiniwa hawakuwa na uelewa kuhusu jinsi kutawaliwa kwa Tanganyika na Wajerumani na baadaye Waingereza kulivyotokea katika karne ya 20. Kielelezo Na.4 kinaonesha sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 43.

43. Kwa nini Tanganyika iliondolewa katika utawala wa Ujerumani na kuwekwa chini ya utawala wa Kiingereza katika karne ya 20?


KWA SABABU YA UKATILI WA WAJERUMANI

**Kielelezo Na.4:** *Sampuli kutoka kwa mtahiniwa aliyeshindwa kubaini matakwa ya swali.*

Aidha, watahiniwa 20,322, sawa na asilimia 2.0, walipata alama 1. Watahiniwa hao waliandika maelezo ambayo hayakustahili alama nzima (2 marks).

Pamoja na hayo, ni watahiniwa 120,074 (11.9%) tu walioweza kupata alama 2. Watahiniwa waliopata alama 2 walieleza kwa ufasaha jinsi kushindwa kwa Ujerumani katika Vita Kuu ya Kwanza ya Dunia kulivyosababisha Tanganyika kuwekwa chini ya utawala wa Kiingereza. Kielezo Na. 5 kinaonesha mfano wa jibu la mtahiniwa aliyekuwa na uelewa kuhusu sababu iliyopelekea

Tanganyika kutawaliwa na Uingereza badala ya Ujerumani katika karne ya 20.



43. Kwa nini Tanganyika iliondolewa katika utawala wa Ujerumani na kuwekwa chini ya utawala wa Kiingereza katika karne ya 20?

Kwa Sababu Wajerumani waashindwa katika vita kuu ya kwanza ya dunia mnamo 1914-1918 Ndio maana utawala wa wajerumani Ukamalizika Tanganyika Mwaka 1919.

**Kielelezo Na.5:** *Sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeweza kueleza sababu zilizosababisha Tanganyika kutawaliwa na Uingereza badala ya Ujerumani katika karne ya 20.*


Soma kwa makini takwimu za mvua katika jedwali lifuatalo kisha jibu swali la 44 na 45.

**Takwimu za Mvua Zilizorekodiwa Mkoani Mtwara Tarehe 12/11/2018 hadi 18/11/2018.**

| Siku | Kiwango cha Mvua |
|---|---|
| Jumatatu | 11 mm |
| Jumanne | 15 mm |
| Jumatano | 13 mm |
| Alhamisi | 20 mm |
| Ijumaa | 10 mm |
| Jumamosi | 5 mm |
| Jumapili | 10 mm |


**Swali la 44**: Taja siku ambazo kiwango cha mvua kilifanana.

Swali hili lilitoka katika mada ya *Hali ya Hewa ya Tarafa, Wilaya na Nchi***.** Watahiniwa walitakiwa kulinganisha viwango vya mvua kutokana na takwimu za mvua zilizorekodiwa katika siku tofauti za juma na kubainisha siku ambazo kiwango cha mvua kilifanana. Kiwango cha ufaulu kwa watahiniwa katika swali hili kilikuwa kizuri kwani watahiniwa 892,063 (88.45%) waliweza kuandika siku za Ijumaa na Jumapili ambazo kiwango cha mvua kilifanana. Hata hivyo, watahiniwa 94,685 (9.4%) walipata alama 0. Chati Na. 25 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali la 44.




**Chati Na. 25:** *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 44.*

Watahiniwa waliopata alama zote (2) mbili waliweza kutoa jibu sahihi kwa kulinganisha viwango vya mvua vilivyorekodiwa katika siku tofauti za juma na kutaja siku ambazo viwango vya mvua vilifanana. Watahiniwa wengi waliweza kujibu kwa usahihi kwasababu swali lilihitaji kulinganisha takwimu zilizopo kwenye jedwali na kutaja siku za juma ambazo kiwango cha mvua kilifanana. Kielelezo Na. 6 ni sampuli ya majibu sahihi ya watahiniwa wenye maarifa ya kutosha kujibu swali hili.



44. Taja siku ambazo kiwango cha mvua kilifanana.

Ijumaa 10 mm

Jumapili 10 mm

**Kielelezo Na. 6***: Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 44*


Kwa upande mwingine, watahiniwa waliopata alama sifuri (0) walishindwa kuelewa matakwa ya swali. Watahiniwa katika kundi hili waliandika siku zisizo sahihi. Hii inaashiria kuwa watahiniwa hawa hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusiana na maswala ya takwimu**.** Kielelezo Na. 7 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kubainisha siku ambazo kiwango cha mvua kilifanana.




**Kielelezo Na. 7**: *Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 44*

**Swali la 45**: Kokotoa wastani wa mvua katika wiki hiyo.


Swali hili lilitoka katika mada ya *Hali ya Hewa ya Tarafa, Wilaya na Nchi*. Swali lilipima uwezo wa watahiniwa katika kusoma na kuelewa takwimu. Katika swali hili, watahiniwa walitakiwa kukokotoa wastani wa mvua kwa siku kutokana na takwimu zilizotolewa. Kiwango cha ufaulu kwa watahiniwa ni kizuri kwani watahiniwa 621,322 (61.61%) walipata alama zote mbili (2). Hata hivyo, watahiniwa 387,150 (38.39%) walipata alama 0 kwasababu walishindwa kuelewa matakwa ya swali hivyo, waliandika majibu yasiyo sahihi. Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 45 umeoneshwa katika Chati Na. 26.




**Chati Na. 26:** *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 45*

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, watahiniwa waliopata alama zote mbili (2) walikokotoa kwa usahihi wastani wa mvua kwa siku kutokana na takwimu za mvua zilizorekodiwa kwa wiki. Watahiniwa hao walijumlisha kiwango cha mvua kilichorekodiwa kwa kila siku na kugawanya kwa idadi ya siku hivyo kupata jibu sahihi ambalo ni mm 12. Kielelezo Na. 8 kinaonesha

sampuli ya majibu ya mtahiniwa mwenye ujuzi na maarifa ya kutosha.


45. Kokotoa wastani wa mvua katika wiki hiyo.

wastani = Jumla / Idadi   $\bar{X}$ = 11mm + 15mm + 13mm + 20mm + 10mm + 5mm + 10mm ÷ 7


$\bar{X}$ = 84mm ÷ 7 .   84/7 = 12

wastani = 12mm

∴ Wastani wa mvua katika wiki hiyo ni mm 12

**Kielelezo Na. 8***: Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 45*

Uchambuzi zaidi umebaini kuwa watahiniwa waliopata alama 0, hawakuwa na maarifa ya namna ya kutafuta wastani. Baadhi ya watahiniwa waliorodhesha tu kiasi cha mvua kilichorekodiwa kwa wiki; wengine hawakujibu kabisa, wakati wengine walitoa majibu yasiyo sahihi. Watahiniwa hawa hawakufanya vizuri kwa kuwa hawakuwa na umahiri wa mahesabu. Kielelezo Na. 6 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kutafuta wastani wa mvua kwa siku.


45. Kokotoa wastani wa mvua katika wiki hiyo.

Wastani wa mvua kwa siku katika wiki 13/15

**Kielelezo Na. 9**: *Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 45*

## 2.0 UCHAMBUZI WA UFAULU WA WATAHINIWA KATIKA KILA MADA

Uchambuzi wa mada zote 27 katika mtihani wa Maarifa ya Jamii unaonesha kutofautiana kwa ufaulu kulingana na mada husika. Ufaulu wa watahiniwa ulikuwa mzuri katika mada 12, wa wastani katika mada 07, na hafifu katika mada 08. Watahiniwa walibainishwa kuwa na kiwango kizuri cha ufaulu kwa kupata asilimia kuanzia 60-100, ambako kumeoneshwa kwa rangi ya kijani katika jedwali. Vilevile, watahiniwa walibainishwa kuwa wamefaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata kati ya asilimia 40-59. Ufaulu katika Jedwali umeoneshwa kwa rangi ya njano. Kwa upande mwingine, ufaulu wa kiwango hafifu ulibainishwa kwa kupata kati ya asilimia 0-39.

Kiwango cha ufaulu huu kimeoneshwa katika jedwali kwa rangi nyekundu.

Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa umeonesha kuongezeka kwa baadhi ya mada, ikilinganishwa na ufaulu wa mwaka 2019. Kumekuwa na ongezeko la ufaulu kutoka kiwango hafifu hadi ufaulu kwa kiwango cha wastani katika mada za *Uhusiano wa jamii za Kitanzania hadi Karne ya 19.* Ufaulu umeongezeka kutoka asilimia 32.8 hadi kufikia asilimia 46.1, na katika*Uvamizi wa Kikoloni katika Afrika kuanzia mwaka 1980,* ufaulu uliongezeka kutoka asilimia 37.6 na kufikia asilimia 40.4. Vilevile, katika baadhi ya mada kiwango cha ufaulu kimeongezeka kutoka kiwango cha wastani hadi kiwango cha kizuri. Mada hizo ni *Ulinzi na usalama katika Shule (*kutoka asilimia 51.95 hadi kufikia asilimia 71.85), *Mawasiliano, biashara na uchukuzi* (kutoka asilimia 58.39 hadi 85.9), *Usomaji wa ramani* (kutoka asilimia 45.63 hadi 61.3) na *Mfumo jua* (kutoka 44.01 hadi 71.4). Kwa upande mwingine, kiwango cha ufaulu wa watahiniwa katika mada ya *Misingi ya Demokrasia* kilishuka kutoka vizuri (84.20%) hadi hafifu (25.2%), *Chimbuko na Mabadiliko ya Binadamu* kutoka wastani (49.00%) hadi hafifu (26.6%), *Alama za shule/Taifa* kutoka vizuri (74.75%) hadi wastani (44.1%), *Uchumi wetu* kutoka (60.47%) hadi wastani (59.75) na *Maji* kutoka vizuri (71.21%) hadi wastani (55.1%).

Kwa ujumla, ulinganifu wa ufaulu wa watahiniwa kwa mwaka 2020 umeonesha kuongezeka ukilinganisha na ule wa 2019. Pia, idadi ya mada zilizoongezeka kiwango cha ufaulu zimeongezeka na idadi ya mada zilizoshuka kiwango cha ufaulu zimepungua. Jedwali Na. 13 linaonesha mada ambazo kiwango cha ufaulu kimeongezeka na Jedwali Na. 14 linaonesha mada ambazo kiwango cha ufaulu kimepungua.

**Jedwali Na. 13: Mada zilizoonesha ongezeko la ufaulu wa watahiniwa**

| Na. | Mada | Wastani wa ufaulu 2019 (%) | Wastani wa ufaulu 2020 (%) | Wastani wa ongezeko (%) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Ulinzi na Usalama katika | 51.95 | 71.85 | 19.9 |

| Na. | Mada | Wastani wa ufaulu 2019 (%) | Wastani wa ufaulu 2020 (%) | Wastani wa ongezeko (%) |
|---|---|---|---|---|
| | Shule/Taifa | | | |
| 2. | Utamaduni wa Tanzania na Tamaduni Nyingie | 18.04 | 35 .40 | 17.36 |
| 3. | Utamaduni Wetu | 79.49 | 80.50 | 1.01 |
| 4. | Shule Yetu | 61.6 | 67.8 | 6.2 |
| 5. | Uhusiano wa Jamii za Kitanzania na Jamii Nyingine za Kiasia na Kizungu | 32.8 | 46.1 | 13.3 |
| 6. | Kuanzishwa kwa Utawala wa Kikoloni katika Africa | 17.17 | 30.65 | 13.48 |
| 7. | Uvamizi wa Kikoloni katika Afrika kuanzia mwaka 1880 | 37.6 | 40.4 | 2.8 |
| 8. | Ushirikiano wa Kimataifa | 14.5 | 24.3 | 9.8 |
| 9. | Mazingira | 55.1 | 66.6 | 11.5 |
| 10. | Mfumo wa Jua | 44.01 | 71.4 | 27.39 |
| 11. | Usomaji wa Ramani | 45.63 | 61.3 | 15.67 |
| 12. | Mawasiliano, Biashara na Uchukuzi | 58.39 | 85.9 | 27.51 |

**Jedwali Na 14: Mada zilizoonesha kushuka kwa ufaulu wa watahiniwa**

| Na. | Mada | Wastani wa ufaulu 2019 (%) | Wastani wa ufaulu 2020 (%) | Wastani wa kushuka (%) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania | 34.77 | 22.41 | 12.36 |
| 2. | Misingi ya Demokrasia | 84.20 | 25.18 | 59.02 |
| 3. | Alama za Shule/Taifa | 74.75 | 44.07 | 30.68 |
| 4. | Chimbuko na Mabadiliko ya Binadamu | 49 | 26.9 | 22.1 |
| 5. | Maji | 71.24 | 55.1 | 16.14 |
| 6. | Shughuli za Kiuchumi | 76.2 | 64.7 | 11.5 |

Muhtasari wa viwango vya ufaulu katika kila mada zilizotahiniwa mwaka 2020 zimeoneshwa katika kiambatisho.

## 3.0 HITIMISHO

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika mtihani wa Maarifa ya Jamii umeonesha kuongezeka kwa kiwango cha ufaulu kwa watahiniwa kwa asilimia 5.10. Kiwango cha ufaulu wa watahiniwa kwa mwaka 2019 kilikuwa asilimia 76.63 na kwa mwaka 2020 kiwango cha ufaulu ni asilimia 81.73.

Kiwango cha ufaulu wa watahiniwa kimeongezeka katika mada ya *Uhusiano wa jamii za Kitanzania na Jamii nyingine za Kiasia na Kizungu* na *Uvamizi wa Kikoloni katika Afrika kuanzia mwaka 1980* kutoka hafifu hadi kiwango cha wastani. Vilevile, ufaulu umeongezeka kutoka kiwango cha wastani hadi kiwango kizuri katika mada za *Ulinzi na usalama katika Shule, Mawasiliano, biashara na uchukuzi*, *Usomaji wa ramani* na *Mfumo wa jua*.

Kwa upande mwingine, kiwango cha ufaulu wa watahiniwa katika mada nne kilipungua. Mada hizo ni *Misingi ya Demokrasia*, *Chimbuko na Mabadiliko ya Binadamu*, *Alama za shule/Taifa*, *Uchumi wetu* na *maji.*

## 4.0 MAPENDEKEZO

Ili kuboresha zaidi kiwango cha ufaulu wa watahiniwa katika somo la Maarifa ya Jamii, Baraza la Mitihani la Tanzania linapendekeza mambo yafuatayo:

(a) Ufundishaji na ujifunzanji wa mada zilizobainika kuwa na ufaulu hafifu ambazo ni *Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania*, *Misingi ya Demokrasia, Utamaduni wa Tanzania na Tamaduni Nyingine, Chimbuko na Mabadiliko ya Binadamu, Kuanzishwa kwa Utawala wa Kikoloni katika Tanganyika na Zanzibar, Kuanzishwa kwa Utawala wa Kikoloni katika Afrika, Harakati za Kupigania Uhuru Afrika na Ushirikiano wa Kimataifa* uzingatie mbinu mbalimbali za ufundishaji ikiwa ni pamoja na;

(i) Kufanya ziara za kimasomo ili kuwawezesha wanafunzi kujifunza katika mazingira halisi ili kuwapa hamasa ya kujifunza zaidi.

(ii) Kuandaa maigizo na kuwashirikisha wanafunzi katika michezo mbalimbali kama njia ya ziada katika ufundishaji na ujifunzaji wa mada kama *Misingi ya Demokrasia* na *Utamaduni wa Mtanzania na Tamaduni Nyingine*.

(iii) Kutumia ya vikundi vya majadiliano ili kumjengea mwanafunzi kumbukumbu ya kudumu.

(iv) Kutumia njia ya kazi mradi (kutegemeana na aina ya mada) katika kukazia maarifa wanayojifunza wanafunzi.

(v) Kutumia njia ya mdahalo wakati wa kujifunza mada mbalimbali ili kujenga ufahamu juu ya mada hizo.

(vi) Kuwaalika wageni/wataalamu waalikwa wa mada mbalimbali.

(vii) Kutumia michoro, ramani na picha mbalimbali kufafanua dhana tofautitofauti wakati wa ufundishaji na ujifunzaji.

(b) Walimu na wanafunzi wapitie taarifa ya uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi inayotolewa na Baraza la Mitihani la Tanzania ili kutambua makosa yanayosababisha kushindwa kufanya vizuri mitihani ya mwisho na kuyarekebisha ipasavyo.

(c) Wanafunzi washauriwe na kusisitiziwa kusoma kwa bidii vitabu vya kiada na ziada ili kuongeza maarifa na ujuzi ambao utawawezesha kujibu maswali ya mtihani kwa usahihi.

(d) Walimu wawapatie wanafunzi mazoezi ya mara kwa mara na kazi za kufanya wanapokuwa darasani na nje ya eneo la shule ili kuwajengea mazoea ya kujisomea mara kwa mara.

(e) Mamlaka husika ziendelee kufanya ufuatiliaji katika ufundishaji na ujifunzaji wa masomo ya Uraia, Historia na Jiografia. Pia kuwashawishi walimu kubadilishana uzoefu kwa kuendesha mafunzo baina yao hasa kuhusu mada zinazooneka kutofanywa vizuri mara kwa mara.

(f) Mamlaka husika zifanye utafiti wa kubaini changamoto zinazozuia ufanisi katika ufundishaji na ujifunzaji na kuziondoa ili kuongeza kiwango cha ufaulu.

**KIAMBATISHO**

**Ulinganifu wa ufaulu kwa watahiniwa katika kila mada kwa mwaka 2019 na 2020**

| Na | Mada | PSLE 2019 | | | | PSLE 2020 | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Ufaulu kwa kila Swali | | (%) Wastani wa Kufaulu | Maoni | Ufaulu kwa kila Swali | | (%) Wastani wa Ufaulu | Maoni |
| | | Namba ya swali | (%) ya Ufaulu | | | Namba ya swali | (%) ya Ufaulu | | |
| 1. | Uongozi katika ngazi ya Mtaa/ Kijiji | - | - | - | - | 1 | 84.82 | 84.82 | Vizuri |
| 2. | Serikali za Mtaa | - | - | - | - | 2 | 62.26 | 62.26 | Vizuri |
| 3. | Uongozi wa Serikali za Mitaa | 2 | 11.48 | 11.48 | Hafifu | - | - | - | - |
| 4. | Serikali Kuu | 12 | 58.31 | 58.31 | Wastani | - | - | - | - |
| 5. | Demokrasia | 5 | 51.95 | 51.95 | Wastani | 3 | 43.9 | 43.9 | Wastani |
| 6. | Alama za Shule/ Taifa | 1 | 74.75 | 74.75 | Vizuri | 5 | 44.1 | 44.1 | Wastan |
| 7. | Ulinzi na Usalama katika Shule/Taifa | 6 | 38.32 | 51.95 | Wastani | 11 | 88.5 | 71.85 | Vizuri |
| | | 11 | 68.58 | | | 9 | 55.2 | | |
| 8. | Uchumi Wetu | 10 | 60.47 | 60.47 | Vizuri | 41 | 63.0 | 59.75 | Wastani |
| | | | | | | 8 | 56.5 | | |
| 9. | Utamaduni Wetu | 9 | 79.49 | 79,49 | Vizuri | 6 | 80.5 | 80.5 | Vizuri |
| 10. | Ushirikiano kati ya Tanzania na Mataifa Mengine | 7 | 48.58 | 48.58 | Wastani | 10 | 50.1 | 50.1 | Wastani |
| 11. | Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. | 4 | 14.18 | 34.77 | Hafifu | 7 | 22.4 | 22.4 | Hafifu |
| | | 41 | 69.53 | | | | | | |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 12. | Misingi ya Demokrasia | 3 | 84.20 | 84.20 | Vizuri | 4 | 25.2 | 25.2 | Hafifu |
| 13. | Utamaduni wa Tanzania na Tamaduni Nyingine | 8 | 18.04 | 18.04 | Hafifu | 12 | 35.4 | 35.4 | Hafifu |
| 14. | Familia Yetu | 14<br>15 | 80.7<br>81.2 | 80.95 | Vizuri | - | - | - | - |
| 15. | Shule Yetu | 16 | 61.6 | 61.6 | Vizuri | 21 | 67.8 | 67.8 | Vizuri |
| 16. | Kijiji Chetu | 18 | 40.8 | 40.8 | Wastani | - | - | - | - |
| 17. | Chimbuko na Mabadiliko ya Binadamu | 23 | 49 | 49 | Wastani | 13<br>19 | 24.2<br>29.6 | 26.9 | Hafifu |
| 18. | Hatua za Maendeleo ya Binadamu Katika Zama Mbalimbali | - | - | - | - | 20<br>42 | 60.9<br>64.7 | 62.8 | Vizuri |
| 19. | Uhusiano wa Jamii za Kitanzania na Jamii Nyingine za Kiasia na Kizungu | 22 | 32.8 | 32.8 | Hafifu | 22 | 46.1 | 46.1 | Wastani |
| 20. | Biashara ya Utumwa | 42 | 21.35 | 21.35 | Hafifu | | | | |
| 21. | Kuanzishwa kwa Utawala wa Kikoloni katika Tanganyika na Zanzibar | - | - | - | - | 43 | 11.9 | 11.9 | Hafifu |
| 22. | Kuanzishwa kwa Utawala wa Kikoloni katika Afrika | 17<br>20<br>21 | 5<br>17.1<br>29.4 | 17.17 | Hafifu | 16<br>17<br>24 | 33.4<br>26.9<br>33 | 30.65 | Hafifu |
| 23. | Vitangulizi vya Kikoloni | 13<br>24 | 26.93<br>33 | 30 | Hafifu | - | - | - | - |
| 24. | Uvamizi wa Kikoloni katika Afrika kuanzia mwaka 1880 | 19 | 37.6 | 37.6 | Hafifu | 15<br>18<br>25 | 46.2<br>28.7<br>46.3 | 40.4 | Wastani |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 25. | Harakati za Kupigania Uhuru Afrika | - | - | - | - | 14 | 25.4 | 25.4 | Hafifuu |
| 26. | Mabadiliko ya Kijamii, Kisiasa na Kiuchumi Katika Afrika Huru | 25.0 | 23.6 | 18.05 | Hafifu | - | - | - | - |
| | | 43 | 12.5 | | | | | | |
| 27. | Ushirikiano wa Kimataifa | 26 | 14.5 | 14.5 | Hafifu | 23 | 30.1 | 24.3 | Hafifu |
| | | | | | | 24 | 28.6 | | |
| | | | | | | 26 | 14.2 | | |
| 28. | Mawasiliano, Biashara na Uchukuzi | 35 | 70.86 | 58.39 | Wastani | 37 | 82.3 | 85.9 | Vizuri |
| | | 36 | 45.93 | | | 38 | 87.9 | | |
| | | | | | | 39 | 87.5 | | |
| 29. | Mazingira | 27 | 44.80 | 55.1 | Wastani | 30 | 92.6 | 66.6 | Vizuri |
| | | 34 | 65.40 | | | 36 | 86.8 | | |
| | | | | | | 40 | 20.7 | | |
| 30. | Shughuli za Kiuchumi | 32 | 64.68 | 76.2 | Vizuri | 29 | 64.7 | 64.7 | Vizuri |
| | | 33 | 87.72 | | | | | | |
| 31. | Usomaji wa Ramani | 44 | 45.97 | 45.63 | Wastani | 31 | 48.5 | 61.3 | Vizuri |
| | | 45 | 45.28 | | | 32 | 70.0 | | |
| | | | | | | 33 | 58.1 | | |
| | | | | | | 34 | 68.6 | | |
| 32. | Maji | 38 | 80.74 | 71.24 | Vizuri | 35 | 55.1 | 55.1 | Wastani |
| | | 39 | 61.74 | | | | | | |
| 33. | Mfumo wa Jua | 31 | 28.92 | 44.01 | Wastani | 27 | 71.4 | 71.4 | Vizuri |
| | | 37 | 74.72 | | | | | | |
| | | 40 | 28.38 | | | | | | |
| 34. | Hali ya hewa | 30 | 68.49 | 68.49 | Vizuri | - | - | - | - |
| 35. | Tafsiri ya Picha na ramani | 28 | 86.03 | 86.02 | Vizuri | - | - | - | - |
| | | 29 | 86.00 | | | | | | |
| 36. | Majanga | - | - | - | - | 28 | 63.3 | 63.3 | Vizuri |